SUPA JACKPOT
TZS.1,087,305,640
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

## MWANAFUNZI auawa madai ya kuiba duka la M-pesa


Siku ya Wanawake Duniani
Daktari aliyepata saratani ya matiti, asimulia siku alivyopokea vipimo
SAMIA: RAIS WA MAFANIKIO NDANI NA NJE
Kuingia kazini tu, akaanza kung'ara kitaifa na kimataifa 'kazi ikaendelea'
• Bajeti ya tabasamu; akadhibiti UVIKO-19
• Siasa kaimudu, sifa yake 'mama hana shida'

UKURASA 11

# Nipashe

Jumatano Machi 8, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581243

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



Rais Samia

Catherine Ruge

### SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

# Wachambuzi watoa neno Rais Samia mkutano wa BAWACHA

UKURASA 2

UKURASA 2

## ... Azidi kung'ara medani za kimataifa





UKURASA 3

Wananchi wakiangalia mabaki ya basi la abiria aina ya Tata mali ya kampuni ya Komba's lililopata ajali baada ya kutumbukia bondeni wakati likipanda Mlima Nkondwe wilayani Tanganyika mkoani Katavi jana. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

## Ajali ya basi ilivyoua watu tisa, kujeruhi wengine 30

SPECIAL SUPPLEMENT ON COMPLETION OF TWO YEARS UNDER THE ABLE LEADERSHIP OF



HER EXCELLENCY DR. SAMIA SULUHU HASSAN

The Guardian Limited will publish a special supplement with **"The Guardian"** and **"Nipashe"** Newspapers, with a special report focusing on the achievements of the Government under the leadership of President **Dr. Samia Suluhu Hassan**

**20th March 2023**

We wish to invite you to be a part of this special supplement by publishing your **Special features, Congratulatory messages, Advertorials** and **Advertisements.**

The Guardian Nipashe

TO BOOK YOUR SPACE PLEASE CALL US TODAY ON +255 677 020 701

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com

61730910I

MICHEZO YANGA: BAMAKO HAWATOKI LEO UK. 24

KATUNI UK. 6

# Wachambuzi watoa neno Samia mkutano BAWACHA

**Na Christina Mwakangale**

BAADHI ya wachambuzi wa kisiasa wamesema kitendo cha Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mgeni rasmi Siku ya Wanawake Duniani pamoja na Baraza la Wanawake la CHADEMA (BAWACHA) leo, kinahitaji kuungwa mkono kwa kuwa kuwapo kwake kunatafsiri umuhimu wa kukaa meza moja bila kujali tofauti za kiitikadi.

Kadhalika, wamesema rais anahitaji kupongezwa kwa utashi wake binafsi usio wa kisheria na kwamba hatua kubwa ni Katiba mpya, hivyo matendo hayo yarasimishwe rasmi kwenye sheria 'mama' kwa kuhakikisha upatikanaji Katiba hiyo chini ya uongozi wake.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, akizungumza na Nipashe jana, alisema tofauti za vyama kisiasa ni kutokubaliana kwa baadhi ya masuala, hakumaanishi kutoshirikiana, akisema upinzani wa kisiasa pamoja na kuwapo mirengo tofauti kwenye vyama vya siasa, unahitaji ushirikiano.

"Upinzani haimaanishi kutokuwa pamoja, lakini wanasiasa wanapaswa kushirikiana wakati wote, hata kama wana malengo tofauti. Kundi moja, fulani linapokuwa madarakani lingine lililobaki liendelee kufanya siasa, haipaswi kuonekana ni uadui.

Anachotuonyesha rais siasa za vyama vingi sio uadui. Makundi yote yanayokosoa, tukiwamo asasi za kiraia, haki za binadamu, hatupaswi kuonekana ni maadui, watu wengine wamekuwa wakituelewa vibaya na tukionekana kama ni maadui," alisema Olengurumwa.

Alisema kwamba kutokana na vyama vya siasa pamoja na asasi hizo kuwa ni Watanzania, bila kujali utofauti kwenye shughuli zao kisekta, uamuzi wa rais umelenga kuleta mabadiliko ya nchi kwa pamoja na kwa kushirikiana na kufuta dhana ya uadui kutokana na itikadi.

"Kuna kipindi fulani kilichopita, mwandishi wa habari alionekana adui, mtetezi wa haki za binadamu adui, vyama vya upinzani walionekana maadui, anachokirekebisha rais ni dhana ya kuwaona watu wengine ni maadui katika taifa letu," alisema Olengurumwa.

Kwa mujibu wa Olengurumwa, hatua hiyo ya rais iwe ni mwanzo kwa viongozi wengine kuiga, akisema tofauti za kiitikadi zisiwafanye Watanzania kutoka meza moja ya ujenzi wa maendeleo.

"Kuwa na itikadi tofauti kusitufikishe kuwa na mitazamo tofauti, tushindwe kukaa meza moja, tukala na wakati mwingine unakuta mwanasiasa anaweza kuwa mume ni chama fulani, mke mimi chama fulani, lakini wako nyumba moja wanakula pamoja. Imekwishatokea wanasiasa fulani wake zao walikuwa vyama fulani ila wako pamoja," alisema Olengurumwa akiongeza:

"Kikubwa hii nia yake, atuletee Katiba mpya kwa sababu ni nia inayofanyika kutokana na utashi wake mwenyewe sio wa kisheria, sio wa kimfumo, ili kurasimisha mema anayoyafanya ahakikishe Katiba mpya inapatikana."

Mchambuzi wa masuala ya kisiasa, Abdulkarim Atiki alisema hatua hiyo ya rais inatafsiri alichokisema kuwa anataka maridhiano, tangu alipoingia madarakani, akisema heshima hiyo aliyopewa na BAWACHA, iwe tunu kwa wanawake wa Kitanzania.

"Rais wetu ni mwanamke, bila shaka hatawaangusha, shida za wanawake kimsingi ni moja, hatuwezi kusema tuwatue ndoo, kwani wanawake sio wakubebeshwa mizigo! Shida za wanawake ni za rais pia. Amejipambanua awali alipoingia alionesha sura yake halisi," alisema Atiki. Kwa mujibu wa mchambuzi huyo, kitendo hicho kiungwe mkono na kisichukuliwe kama ni jukwaa la kisiasa, badala yake itazamwe sura ya maridhiano na ujenzi mpya wa nchi bila kujali tofauti za kikabila wala kiitikadi.

Abbas Mwalimu, ambaye ni mchambuzi wa kisiasa, alisema hatua hiyo tafsiri yake ni uhimilivu na uwezo wa mfumo katika kusimama hata palipo na misukosuko, mfadhaiko na kuleta hali nyingine na tabia mpya.

"Kwa mfano, Holing (1973:14) alitafsiri ustahimilivu au uhimilivu kama kipimo cha uwezo wa mfumo kuendelea kushikilia ilichoshika na uwezo wake wa kukubaliana na mabadiliko na usumbufu na bado mfumo ukaendelea kuwa katika uhusiano uleule na jamii ya watu na vigezo vilivyowekwa na serikali.

"Uhimilivu unaakisi uwezo wa mtu au taasisi kukabiliana na changamoto na kubaki katika tabia na mwenendo uleule wa kibinadamu au utu. Berkes na wenzake walisema kuwa pamoja na mabadiliko bado ukabakia na udhibiti uleule wa mambo ya msingi katika utendaji na muundo wake," alisema Mwalimu.

Alisema kutokana na tafsiri hizo, kisiasa inabainika kwamba demokrasia inapaswa iwaunganishe watu na sio kuwagawa kama ambavyo ilianza kuonekana nchini na iwe chanzo cha vyama mbadala kuibua hoja makini dhidi ya chama kinachoongoza.

"Mtazamo huu wa Rais Samia unatokana na kutambua kwamba 'standard' (kiwango) ya mikataba ya kimataifa inatambua msingi wa demokrasia katika sura hiyo, Ibara ya 21 ya Tamko la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa (Universal Declaration of Human Rights-UDHR) hayo," alisema Mwalimu.

Kadhalika, aliitaja demokrasia sio chuki, uadui, matusi na wala sio dhihaka dhidi ya mtu au chama fulani, bali ni uwezo wa mfumo kustahimili, kuishi na kupona kutokana na changamoto na magumu ambayo huleta mfadhaiko au shinikizo ambalo linaweza kusababisha kushindwa.



"Sichukulii wapinzani kama maadui, nawachukulia kama watu watakaonionesha changamoto zilizopo nizitekeleze, ili CCM iimarike. Rais Samia anaonesha wazi kuwa misingi ya demokrasia ni pamoja na kuthamini michango na maoni ya wengine katika kumfanya yule aliyopo madarakani kutekeleza sera kiubunifu zaidi," alisema Mwalimu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga alisema kwamba, Rais Samia, ameonesha ni kwa namna gani alivyokomaa kidemokrasia.

"Inamaanisha kwamba Rais Samia kakomaa kidemokrasia. Maana vyama vingi sio uadui," alisema Anna.

**LISSU AFUNGUKA**

Lissu alisema: "Kwanza naomba niseme sikumbuki katika Tanzania ya vyama vingi, Mwenyekiti wa CCM ambaye ni rais wa nchi amewahi kushiriki katika shughuli rasmi iliyoandaliwa na chama cha upinzani hasa chama kikuu.

"Huyu Rais anahitaji kutiwa moyo na amepata 'confidence' (ujasiri) ya CHADEMA kwamba mwelekeo wake ni mzuri, tumemwalika kwa sababu hiyo, ni mgeni wa BAWACHA kwa sababu amefanya mambo ambayo marais wengine walipita hawakuyafanya."

"Kama chama tunapata jukwaa la kuzungumza na Watanzania wote na dunia kwa sababu vyombo vyote vya habari vitakuwa hapo, ni wajibu wetu tunaomwalika, kulitumia hilo jukwaa, dhambi haitakuwa ya rais itakuwa yetu."

## ... Azidi kung'ara medani za kimataifa

**Na Restuta James**

WAKATI dunia ikiadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake leo, baadhi ya wasomi na wanasiasa wamepongeza utendaji wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wakieleza kuwa ni kiongozi anayeunganisha nchi katika sekta nyingi hasa kisiasa.

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam, Mchumi Mwandamizi, Dk. Donath Olomi, alisema maridhiano ya kisiasa yanayofanywa na Rais Samia yataijenga Tanzania na kufungua mifumo mingi.

Alisema maridhiano yatawaweka watu wengi huru na kwamba uhuru ni chanzo cha haki za msingi katika kuijenga nchi.

"Ni jambo la msingi hata katika kupata maendeleo mengine watu wanapokuwa na uhuru wa fikra...anaweka mazingira yanayoashiria haki ambayo ndio msingi unaoweza kujenga amani tunayoihitaji kwa ajili ya maendeleo," alisema.

Dk. Olomi alisema maridhiano ni jambo muhimu ambalo lilihitajika kufanyika nchini.

'R' nne anazozisimamia ni Reconciliation (Maridhiano), Resiliency (Ustahamilivu), Reforms (Mabadiliko) na Rebuilding (Kujenga upya).

Mbunge wa zamani wa Kahama (CCM), James Lembeli, alisema maridhiano yanayofanywa na Rais Samia ni jambo la kuungwa mkono na wapenda haki, demokrasia na maendeleo.

Hata hivyo, alitahadharisha kwamba ndani ya Chama Cha Mapinduzi wako baadhi ya makada ambao wanapenda kujikomba na siasa za unafiki.

"Aliingia madarakani wakati nchi ikiwa kwenye tension kubwa...uendeshaji wa serikali iliyopita uliwagawa watu hata serikalini kulikuwa na malalamiko mengi. Hekima ya Rais Samia aliona kwamba hawezi kuongoza nchi ambayo iko kwenye vipande vipande," alisema.

"Akafikiria namna ya kuendesha nchi kwa amani, mshikamano na watu kuzungumza...ndani ya CCM bado kuna tatizo la unafiki. Pamoja na kwamba anachukua hatua nzuri wapo ambao hawapendi," aliongeza.

Lembeli alisema kitendo cha Mwenyekiti wa CCM kuwa mgeni rasmi kwenye sherehe za BAWACHA kunaashiria jambo linaloashiria moyo wake wa kuunganisha nchi.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema mageuzi yanayofanywa na Rais Samia yanaiweka Tanzania kwenye taswira nzuri duniani.

Alisema wanasiasa wanafurahia 'R' nne za Dk. Samia kwa kuwa zinarudisha siasa katika uwanja mzuri akieleza kuwa kauli ya Rais kusema siasa sio uadui ni kauli nzito na muhimu.

Alisema 'R' nyingine ni michakato inayoendelea na kwamba matokeo yake yanaonekana.

**ATAJWA KIMATAIFA**

Wadadisi wa masuala ya kisiasa wameiambia Nipashe kwamba utendaji wa Rais Samia umeiweka Tanzania kwenye ramani nyingine duniani kwa kuwa ametajwa na taasisi za kimataifa kuwa miongoni mwa watu wenye ushawishi mkubwa.

Hii ni kutokana na Desemba mwaka jana Taasisi ya The Royal Al Al-Bayat Institute for Islamic Thought (RABIIT), kumtaja kuwa miongoni mwa watu mwenye ushawishi mkubwa duniani.

Katika orodha ya watu 500 wenye ushawishi zaidi duniani iliyotolewa na RABIIT, Dk. Samia anashika nafasi ya 38 mbele ya mshambuliaji wa klabu ya Liverpool na timu ya Taifa ya Misri, Mohamed Salah.

Rais Samia ametajwa na Forbes kwa miaka miwili mfululizo kuwa miongoni mwa wanawake 100 wenye ushawishi zaidi duniani.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanaeleza kuwa hakutajwa kwa upendeleo bali kwa haki kutokana na namna anavyoyaweka kwenye vitendo anayoyasema.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo, akizungumza na wananchi wa kijiji cha Litula juzi, ambapo amewataka wazazi wanawake kuacha tabia ya kuwawekea vijiti vya uzazi wa mpango watoto wao wenye umri wa chini ya miaka 18, kwani kufanya hivyo ni sawa na ukatili wa kijinsia. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Ajali ilivyoua watu tisa na kujeruhi 30

**Na Neema Hussein,** MPANDA

WATU tisa wamefariki dunia na wengine 30 kujeruhiwa katika ajali ya gari iliyotokea kwenye mlima mkali wa Nkondwe, wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi.

Ajali hiyo ilitokea baada ya basi la abiria aina ya Tata lenye namba za usajili T506 DHH kampuni ya Komba's, lililokuwa likitokea mkoani Kigoma kwenda Mpanda mkoani Katavi kuacha njia na kutumbukia bondeni.

Taarifa ya Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, Dk. Alex Mrema, ilisema vifo hivyo tisa vilitokea papo hapo na waliofariki dunia ni wanaume watano wakiwamo watu wazima wawili na watoto watatu .

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame, alisema ajali hiyo ilitokea baada ya gari hilo kufika katika mlima huo na gari kuserereka na kudondokea kwenye bonde kubwa lenye kina cha mita zisizopungua 75.

Alisema hadi taarifa zinatolewa chanzo cha ajali kilikuwa bado hakijajulikana na Jeshi la Polisi lilikuwa linaendelea na uchunguzi huku kazi ya kuitambua miili ikiendelea kwa ajili ya taratibu zingine.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, akiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika kuwajulia hali majeruhi wanaoendelea kupatiwa matibabu, alisema serikali imeguswa na ajali hiyo huku akitoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa waliopoteza maisha. Mrindoko alisema kutokana na vifo hivyo, taifa limepoteza nguvu kazi.

"Kuna baadhi walikuja wakiwa na hali si nzuri lakini mara baada ya kupata matibabu hapa hospitalini, Tanganyika tayari hali zao zimeendelea kuimarika. Tuendelee kuwaombea waliopata majeraha wapone haraka," alisema Mrindoko. Mmoja wa majeruhi katika ajali hiyo, Philbert Focus, mkazi wa Mpanda, alisema wakati wamefika katika mlima huo, ghafla kwenye kona gari lilikwenda kwa kasi kubwa kama limekatika breki ndipo lilipomshinda dereva na kupitiliza hadi bondeni.

"Niliona kama giza baadaye nikawa nimefumbua macho nikajikuta naumia nipo ndani gari limelala juu chini nikajikwamua kutoka japo kulikuwa na kanafasi kadogo. Maumivu niliyopata ni ya mkono na michubuko kichwani na mguuni," alisema Focus.

Hamadi Kambi shuhuda wa ajali hiyo, ambaye alikuwa katika harakati za kushirikiana na Jeshi la Polisi kuokoa majeruhi, alisema ajali ilikuwa mbaya na kwamba watu wanne wamefia mikononi mwake wakati wa mchakato huo.

"Kuna mtoto mama yake kanifia mikononi, yule mtoto kanisikitisha sana," alisema Kambi.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Mwenyekiti wa Mtaa wa Luhafwe, Raphael Lutonja, alisema eneo hilo ni baya sana na mara kadhaa kumekuwa kukitokea ajali na kusababisha vifo huku akisema ajali iliyotokea jana ni mbaya zaidi kuliko ajali ambazo zimewahi kutokea eneo hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Onesmo Buswelu, aliwashukuru wananchi kwa kusaidiana na serikali katika uokoaji na kujitolea vyombo vya usafiri kwa ajili ya kuwapeleka majeruhi hospitalini.

# Mwanafunzi auawa madai kuiba duka la M-Pesa

**Na Mwandishi Wetu,** MBOZI

MWANAFUNZI wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari ya Kutwa ya Ndugu, Mbozi mkoani Songwe, Daud Simkoko (17), ameuawa kwa kipigo kisha kuchomwa moto na wananchi kwa tuhuma za wizi katika duka la huduma za kifedha.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Rashid Ngonyani, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo ingawa hakuwa tayari kueleza kama Simkoko alikuwa mwanafunzi lakini taarifa za uhakika kutoka katika vyanzo mbalimbali zimethibitisha kuwa alikuwa mwanafunzi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, Kamanda Ngonyani alisema tukio hilo lilitokea Machi 5, mwaka huu, majira ya saa 5:03 usiku katika eneo la Soko Kuu, mjini Vwawa, wilayani Mbozi.

"Mtuhumiwa (marehemu) alikamatwa na walinzi wa maduka kwa kushirikiana na wananchi akiwa ndani ya duka la miamala ya kifedha linalofahamika kama Kapamato akiwa amekata sehemu ya bati la paa la jengo hilo na kuingia ndani kwa lengo la kuiba," alisema.

Ngonyani alisema kijana huyo aligunduliwa na walinzi baada ya kuwakurupua wenzake wawili waliokuwa nje na ambao walikimbia na kumwacha akiwa ndani ya jengo.

"Walinzi baada ya kuona hivyo, walipuliza filimbi kwa lengo la kuomba msaada na mtuhumiwa alipojaribu kukimbia, walinzi kwa kushirikiana na wananchi waliojitokeza, walifanikiwa kumkamata na kuanza kumshambulia na kisha kumchoma moto," alisema Ngonyani.

Alisema polisi walipata taarifa na askari waliokuwa doria walipofika eneo la tukio, walikuta tayari mtuhumiwa huyo alikuwa amefariki dunia.

Kwa mujibu wa Ngonyani, Simkoko baada ya kutoboa bati na kuingia ndani, aliharibu mfumo wa kamera ya mfumo wa ulinzi (CCTV) uliokuwa umefungwa ndani ya duka hilo.

Pia Kamanda Ngonyani alisema kabla ya tukio hilo, kijana huyo tayari alikuwa anatuhumiwa kwa matukio ya wizi kwa kutumia mbinu hiyo hiyo ya kutoboa bati na kuingia ndani.

Alisema Januari 18, mwaka huu, alikamatwa kwa wizi katika maduka matatu katika mtaa wa Ilembo, wilayani Mbozi na kuiba Sh. 2,358,000 na vitu vingine kama simu sita za mkononi na mafuta ya kupaka aina ya Family.

"Mtuhumiwa baada ya kuhojiwa, alikiri kutenda kosa hilo na kufikishwa mahakamani kwa kesi kumbukumbu namba JUV.01/2023 kosa kuvunja duka usiku na kuiba," alisema Ngonyani.

Uongozi wa Shule ya Sekondari ya Ndugu ulipoulizwa kuhusu mwanafunzi huyo, ulithibitisha kuwa ni miongoni mwa wanafunzi wa kidato cha nne na kwamba tengu Januari, mwaka huu, hakuwa shuleni baada ya kushtakiwa mahakamani kwa madai ya wizi.

"Daud (marehemu) alikuwa mwanafunzi wetu na kwa mara ya mwisho aliripoti hapa Januari na baadaye akapata tatizo ambalo tulimsimamisha mpaka atakapolimaza na mwezi huu bodi ya shule ilitaraji kukutana na moja ya mambo ya kujadili lilikuwa suala lake. Lakini katika mshangao mkubwa, tumepokea taarifa za kuuawa kwake," alisema mmoja wa viongozi wa shule aliyeomba jina lake lihifadhiwe.


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO KWA WADAIWA WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi wote wanaodaiwa viwanja katika maeneo ya Mtumba, Michese, Nzuguni, Kitelela, Kikombo, Iyumbu, Nzuguni Bus Stand, Nala Industrial Area, Njedengwa Investment Area, Nala, Chahwa, Iyumbu New Town Centre, Mahomanyika, Vikonje, Nala Chigongwe, Ihumwa, Mapinduzi, Medeli, Nala lugala, Nala Segu kukamilisha malipo ya viwanja hivyo mapema.

Mwananchi au taasisi itakayoshindwa kulipia kiwanja hadi kufikia tarehe 25 Machi, 2023 atambue kuwa kiwanja hicho kitauzwa kwa mteja mwingine ili kuboresha huduma katika Halmashauri bila kutoa taarifa yeyote kwa mteja wa awali.

**Tangazo hili limetolewa na:**

Joseph C. Mafuru
**MKURUGENZI WA JIJI**
**DODOMA**

MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
S. L. P. 1249,
DODOMA

217303602

# Spika akumbushia uhalali wa kina Mdee kuendelea bungeni

**Na Elizabeth Zaya**

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amesema bunge linasubiri uamuzi wa mahakama ili kuamua hatima ya wabunge 19 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kubaki au kuondolewa katika chombo hicho.

Dk. Tulia alisema hayo jana wakati akihojiwa na chombo kimoja cha habari kuhusu sababu za wabunge hao kuendelea kuwapo bungeni ilihali chama chao kinadai kuwafukuza.

"Kikatiba, hakuna mtu anayeweza kuwa mle ndani (bungeni) ukiacha Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Swali linaulizwa mbona hawa chama chao kilishawafukuza halafu bado wako bungeni?

"Bado wako bungeni kwa sababu wamekwenda mahakamani na sisi tunasubiri mahakama ifanye uamuzi. Kwa nini tumetoa nafasi ya mahakama kufanya uamuzi? Kwa wale wanaofuatilia kesi hizi za kisiasa, wabunge walioko bungeni si wa kwanza kubaki baada ya vyama vyao kutangaza kuwa vimewafukuza.

"Walishakuwako huko zamani wabunge ambao wameshawahi kwenda mahakamani. Hamad Rashid wa Zanzibar alishawahi kufukuzwa kwenye chama chake lakini aliendelea kuwapo kwa sababu kesi ilikuwa inaendelea mahakamani. "Zitto Kabwe alishawahi kupitia mazingira hayo kwa hiyo wako wabunge wengi tu ambao hata vyombo vya habari viliwaita wabunge wa mahakama," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Tulia, endapo mahakama itatoa uamuzi kwamba walifukuzwa kihalali katika kipindi hiki ambacho bado wako bungeni, watafukuzwa lakini akabainisha kwamba hawawezi kuipangia mahakama namna ya kuendesha shughuli zake.

"Ukiwatoa hawa halafu mahakama ikaja kusema chama chao kiliwafukuza kihalali, hakuna anayepoteza chochote hapo. Kwa hiyo na wao wanakuwa si wabunge kama mahakama itatoa uamuzi ndani ya kipindi hiki ambacho bado wako bungeni wataondoka. "Wako bungeni kwa sababu mahakama haijasema kwamba kesi hii imefikia mwisho. Ikisema hawa watu wamefukuzwa kihalali wanaondoka bungeni au hawa watu chama hakikufuata utaratibu mzuri, sasa kitafuata utaratibu mzuri wa kuwaondoa halafu wataondoka bungeni," alisisitiza.

Dk.Tulia alisema bunge linasubiri mahakama itafsiri utaratibu ambao chama cha wabunge hao kiliutumia katika kuwafukuza.

"Katiba yetu imeweka mgawanyo wa madaraka na sisi tunatunga sheria zinatafsiriwa na mahakama. Kwa hiyo tunasubiri mahakama itafsiri utaratibu ambao chama cha hao wabunge kimeutumia, kama itasema wamefukuzwa kihalali, wataondoka bungeni, kama mahakama itatoa uamuzi wakati gani, sisi hiyo sio kazi yetu kuwapangia," aliongeza.

**MNYIKA AMJIBU**

Baada ya Spika kusema hayo, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alijibu kupitia twitter kwamba Spika amepotosha.

"Spika Tulia Ackson amepotosha Hamad Rashid alipata amri ya mahakama ya kubaki Bungeni. Zitto aliomba zuio la mahakama asifukuzwe uanachama baada ya kuvuliwa uongozi. Hawa Wasaliti 19 kwa sasa hakuna 'court injuction' (zuio la mahakama) na pia 'order ya status quo' (amri ya kuendelea na nyadhifa zao) waliyopata awali haipo," aliandika Mnyika.

CHADEMA ilitangaza kuwavua uanachama Halima Mdee na wenzake 18 Novemba 27, 2020 baada ya kwenda bungeni kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalumu wakati viongozi wao wakuu wakidai kutoutambua uchaguzi mkuu na kutovitambua viti hivyo maalumu vya ubunge walivyopata katika uchaguzi huo.

Wabunge hao walifungua kesi Mahakama Kuu kupinga uamuzi wa Baraza Kuu la CHADEMA kuwafukuza uanachama. Kesi hiyo inakuja kesho kwa ajili ya upande wa waleta maombi kuwahoji wajumbe wa baraza.




Meneja Mawasiliano wa Barrick nchini, Georgia Mutagahywa (wa tatu kushoto), akikabidhi msaada wa vifaa vya hospitali kwa Daktari wa Hospitali ya Mwananyamala, Eliyafie Huruma mkoani Dar es Salaam jana, vilivyotolewa na kampuni hiyo katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani. Wengine ni wafanyakazi wa Barrick na hospitali hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chongolo akerwa mashamba kutelekezwa

**Na Augusta Njoji,** MBULU

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amekerwa na kutelekezwa kwa mashamba ya ngano yaliyoko eneo la Basotu mkoani Manyara. Kutelekezwa kwa mashamba hayo kumesababisha uzalishaji mdogo wa ngano na kulazimu kutumika fedha nyingi za kigeni kuagiza nje ya nchi.

Kutokana na hali hiyo, ameagiza Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Kilimo wakubaliane ndani ya siku 14 kukabidhiana mashamba hayo kwa wizara yenye dhamana ya kilimo ili mwaka huu uzalishaji uanze.

Chongolo akizungumza juzi kwenye mkutano wa hadhara na wananchi wa Mbulu mkoani Manyara, akiwa kwenye ziara yake na sekretarieti ya CCM ya kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi 2020-2025, alisema mkoa huo ndio uliokuwa ukizalisha ngano kwa wingi.

"Pale Basotu kuna mashamba makubwa sana. Yale mashamba pamoja na mradi mzima uliochukuliwa na mtu anayeitwa Msajili wa Hazina akakaa nayo mfukoni miaka yote yeye halimi si mkulima.

"Nchi ina uhitaji mkubwa wa ngano na tunalazimika kuagiza ngano nje ya nchi. Mimi nimepita pale jana nimesikitishwa pamekaa kimya hakuna uzalishaji," alisema.

Chongolo alisema haiwezekani kutumia fedha nyingi za kigeni kupunguza akiba ya fedha hizo kwa kuagiza bidhaa hiyo nje ya nchi.

"Tuna mashamba yanayoweza kutuzalishia ngano ya kutosha nchini na kutuondolea changamoto ya fedha yetu ya kigeni kwenda nje. Nimeagiza hilo naamini wanajua umuhimu wa kufanya hivyo na hawatasita kufanya haraka. Wakichelewa mimi nina dhamana ya kuhangaika na hao wanaochelewesha," alisema.

Katibu Mkuu aliwahakikishia mwaka huu ngano itaanza kuzalishwa kwenye mashamba hayo kama ilivyokuwa awali.

Hata hivyo, alisisitiza CCM haiwezi kuwa na watu ambao wamepewa jukumu la kutekeleza yaliyoahidiwa na wananchi kwa kufanya kazi kwa mazoea. "Tunataka watu wakae sawa sawa wajue wana wajibu wa kufanya na kubadilisha matokeo kuwa tija kwa wananchi," alisema.

Kuhusu ujenzi wa daraja linalounganisha Mang'ora na Mbulu, Katibu Mkuu huyo aliagiza kuhakikisha barabara husika itengenezwe ili kupitika wakati wote.

# Ahukumiwa kunyongwa hatia kuua kwa kukusudia

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Mwanza imemwachia huru Reuben Makanika na kumhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa, Lameck Samson baada ya kumtia hatiani kwa kosa la mauaji ya kukusudia.

Hukumu hiyo ilisomwa mbele ya Jaji Mwanabaraka Mnyukwa, baada ya kusikiliza ushahidi wa upande wa Jamhuri na utetezi wa washtakiwa.

Upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi sita na upande wa utetezi ulikuwa na mashahidi wawili.

Katika shauri hilo upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali, Clement Mango, Constantine Ramadhani na upande wa utetezi uliwakilishwa na Innocent Kaijage.

Ilidaiwa Mei 5, 2018 saa tatu usiku maeneo ya Kijiji cha Rumasa, wilayani Chato mkoani Geita, washtakiwa walimuua kwa kukusudia Dotto Ntururu.

Miongoni mwa mashahidi sita, shahidi wa kwanza katika shauri hilo ni Halifa Mshana ambaye ni daktari katika Hospitali ya Wilaya ya Chato tangu mwaka 2015.

Alidai Mei 5, 2018 alikuwa kwenye kituo chake cha kazi na alipangiwa kazi ya kuchunguza mwili wa marehemu Dotto mwenye umri kati ya miaka 40 na 44.

Alidai kuuchunguza mwili wa marehemu na kubaini kuwa kifo kilitokea ndani ya saa 24 na ana majeraha mengi yaliyosababishwa na kitu chenye ncha kali na kulikuwa na jeraha kubwa upande wa kulia wa kichwa na fuvu lilipasuka.

Shahidi huyo alidai kifo kilisababishwa na kupoteza damu na kuvunjika kwa fuvu. Ushahidi unadai mshtakiwa Lameck alimpiga marehemu kwa kutumia jembe na kumuua kisha kuupeleka mwili wake porini.

Pia ilidaiwa baiskeli yake iliachwa kwenye kichuguu na kuondoka nyumbani ambako usiku alikamatwa.

Hata hivyo, katika maelezo ya onyo mshtakiwa wa kwanza alikiri kuhusika katika tukio hilo.

Mahakama baada ya kusikiliza ushahidi wote ilifikia hitimisho kwamba kosa la mauaji dhidi ya Reuben Makanika, halijathibitishwa.

Jaji Mnyukwa alisema hakukuwa na ushahidi wa kutosha wa kumhusisha na kesi ya mauaji na kwamba mshtakiwa huyo anaachiwa huru atolewe gerezani isipokuwa kama atakuwa ameshikiliwa kihalali kwa makosa mengine.

"Kwa upande mwingine, mahakama imejiridhisha kwamba ushahidi wa upande wa mashtaka ni wa kuaminika dhidi ya mshtakiwa wa kwanza Lameck Samson.

"Natamka kwamba upande wa mashtaka umethibitisha kesi yao bila shaka yoyote dhidi ya Lameck.

"Mahakama inamuona Lameck ana hatia kama alivyoshtakiwa kwa hivyo anatiwa hatiani kwa mauaji," alisema Jaji Mnyukwa.

HABARI KITAIFA

# JKCI, Kinondoni waanzisha kambi upimaji afya bure

**Na Pilly Kigome**

MADAKTARI na wataalamu wanawake kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kushirikiana na wataalamu wa Manispaa ya Kinondoni wamefanya upimaji na matibabu ya moyo bure kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.


Upimaji huo ulianza Machi 6 na kumalizika jana katika viwanja vya CCM Mwinjuma Mwananyamala, jijini Dar es Salaam.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, alisema madaktari hao wamefanya kitu kikubwa kuwajali wananchi wa Kinondoni na vitongoji vyake na unaonyesha jinsi wanawake walivyokuwa na upendo na nchi yao. Alitoa wito kwa wakazi wa manispaa hiyo na maeneo ya jirani kujitokeza kwa wingi na kutumia fursa hiyo vizuri kwa kuja kutambua afya zao na kupatiwa matibabu na kupata mwongozo wa kuishi ili kulinda afya zao za moyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa upasuaji JKCI, Anjela Muhozya alisema wameguswa kuona baadhi ya Watanzania wanajitokeza kujua afya zao mapema na kujigundua afya zao.

Alisema sababu nyingine iliyowagusa kufanya vipimo eneo hilo ni kuona watanzania wengi wamekuwa wakishindwa gharama za upimaji na kujitibia afya ya moyo kulingana na gharama kuwa kubwa na kujikuta wakishindwa kufanya hivyo kutokana na hali za kiuchumi.

Mtaalamu lishe kwa Taasisi hiyo, Husna Faraji alitoa elimu elekezi kwa wananchi waliojitokeza katika viwanja hivyo, ili kukabiliana na matatizo hayo ya magonjwa ya moyo ambayo yanakua kwa kasi siku hadi siku kutokana na mfumo wa maisha wa kila siku.




Programu Meneja wa Taasisi ya Zaina Foundation, Shega Mboya, akitoa elimu ya kuhamasisha usawa wa kijinsia kwenye teknolojia katika Kijiji cha Kiromo wilayani Bagamoyo mkoani Pwani juzi, kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake Duniani inayoadhimishwa leo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Jaji: Hakuna haki jinai bila weledi

**Na Ashton Balaigwa,MOROGORO**

JAJI Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Morogoro, Paul Ngwembe, amesema haki jinai haiwezi kupatikana bila kuwapo wapelelezi wenye ujuzi na weledi wanaotoa haki kwa wote.

Amesema haki jinai pia inahitaji kuwapo wapelelezi ambao wako tayari kutumia ujuzi wao kuhakikisha wanaotuhumiwa kufanya makosa wanafikishwa mahakamani na haki yao wanaipata.

Jaji Ngwembe alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa waendesha mashtaka na wapelelezi juu ya upelelezi unaofanikisha mashtaka ambayo yameandaliwa na Mahakama ya Tanzania na kuendeshwa na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mradi wa maboresho awamu ya pili.

"Yako makosa yanayofikishwa mahakamani bila kuwa na upelelezi uliokamilika au kukamata mtuhumiwa na kumshikilia kwenye vituo vya polisi bila kuwapo upelelezi wa dhati unaomhusisha mtuhumiwa," alisema Jaji Ngwembe

Aliainisha makosa yenye adhabu ya vifungo vya muda mrefu yakiwamo ya ubakaji, ulawiti na uhusiano yaliyoharamishwa kwa sheria, yaani wakati mwingine yametumika kudhalilisha watu wasio na hatia, hata ugomvi wa kifamilia husababisha kuhusisha makosa ya namna hiyo.

Kwa mujibu wa Jaji Ngwembe, upelelezi na uendeshaji wa makosa ya jinai ni wa kisanyansi zaidi kuliko hisia na nadharia za kizamani na makosa mengi yanathibitishwa kisanyansi kwa kutumia vinasaba (DNA), vipimo vya kidaktari au kwa kutumia wataalamu wa utambuzi wa maandishi.

"Yapo matumizi mabaya ya vipimo vya kitaalamu kwa kuwatumia watu wasio na utaalamu wa kutosha, hivyo nashawishika kushauri serikali au bunge kutunga kanuni na vigezo kwa hao wataalam wenye uwezo wa kutoa ushauri," alisema.

Wakati huo huo ,Mahakama ya Tanzania inatekeleza Mpango Mkakati wake na imejiwekea viwango vya muda wa mashauri kuwapo mahakamani, yaani mahakama ya mwanzo miezi sita, mahakama za wilaya na hakimu mkazi miezi 12 na mahakama kuu miezi 24.

Alisema kwa mujibu wa ripoti ya Msajili Mkuu wa Mahakama ya Utendaji wa Shughuli za Mahakama kwa mwaka 2021, kulikuwa na mashauri ya mlundikano 4,447 katika mahakama za hakimu mkazi na wilaya na mashauri 1,616 sawa na asilimia 36.3.

Mashauri hayo, alisema ni yale ambayo mahakama hazikuwa na mamlaka ya kuendelea nayo yakisubiri kukamilika kwa upelelezi na kutolewa vibali toka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Alisema katika zama hizi na mapinduzi ya nne ya viwanda, matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ni ya lazima kwa kuwa si tu yataokoa muda na gharama lakini pia yataongeza ubora wa ushahidi.

Jaji Ngwembe aliwakumbusha washiriki hao kuwa wao ni watumishi wa umma na wanaongozwa pamoja na sheria zingine na Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 pamoja na kanuni zake za mwaka 2003 kama walivyo watumishi wengine wa umma.

Kwa mantiki hiyo, aliwataka kuzingatia maadili ya utumishi wa umma, miiko pamoja na maadili yanayoongoza katika utendaji kazi wao .

Baada ya kutajiwa mikoa inayoshiriki na kukosekana kwa mkoa wa Morogoro, Jaji Ngwembe aliwasilisha ombi binafsi kwa IJA kuwaalika washiriki wawili wa mkoa wa Morogoro mmoja kutoka Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi Makosa ya Jinai wa Mkoa na mwingine kutoka Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali.

Naibu Msajili Mwandamizi wa Mahakama Kuu, Arnold Kirekiano, alisema mafunzo hayo ya wiki nne yanayofanyika kwenye Kituo Jumishi cha Utoaji Haki Morogoro yanahusisha washiriki 250 ambao wanashiriki kwa makundi na kwa awamu ya siku tano ni kutoka taasisi mbalimbali zikiwamo Ofisi ya Mashtaka na Jeshi la Polisi.

Kirekiano alisema mafunzo hayo yanawaleta pamoja washiriki ili kubadilishana uzoefu kuhusu utendaji kazi wa kila siku zikiwamo changamoto zinazotokana na kukua kwa teknolojia na kubadilika kwa mbinu za uhalifu na wahalifu.


**TIBA** Tanzania Insurance Brokers Association

**NOTICE FOR AN EXTRAORDINARY GENERAL MEETING**

*DEAR TIBA MEMBERS.*

In terms of section 24.4 (a) of the TIBA Constitution, An Extraordinary General Meeting can be called at any time if for any reason Governing Council deems expedient.

Given that our TIBA constitution needed some review and amendments, the Governing Council hereby serves upon TIBA Members a notice for the Extraordinary General Meeting to review and amend the TIBA constitution as follows;

**DATE:** Thursday 23rd March 2023
**TIME:** From 8.30 AM
**VENUE:** ONOMO Hotel, Ghana Avenue (opposite Exim Tower) Dar es salaam.

**AGENDA:**
1) **To review and Amend the TIBA Constitution of October 2011.**

All members are kindly requested to attend this meeting as the contribution by each member is highly required.

**IMPORTANT:**
1) Please confirm your attendance to the secretariat before March 20, 2023 to enable proper planning of the event.
2) Secretariat contacts are; Email **officeadmin@tiba.co.tz**; cell phone: 0677636722.

**ALIASGHER SOMJI**
**HONORARY SECRETARY**
**06th March, 2023.**

217314002


*1st Floor, NIC Kisutu Branch*
*Plot No. 9 Block "A"*
*Olympio Street (Off Bibi Titi Road)*
*P.O. Box 77042 Dar es Salaam*
*Mobile: +255 677636722*
*E mail: info@tiba.co.tz ; officeadmin@tiba.co.tz*
*Website:www.tiba.co.tz*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanawake wanaweza, waendelee kuungwa mkono

**SIKU** ya Wanawake Duniani huadhimishwa kila mwaka Machi 8. Maadhimisho hayo yaliridhiwa na Umoja wa Mataifa mwaka 1975 kama siku rasmi ya kuikumbusha dunia kuhusu haki za wanawake.
Sherehe ya Siku ya Wanawake huongeza chachu katika harakati za mapambano katika usawa wa kijinsia kwa pande zote wanawake na wanaume katika jamii.
Siku hii muhimu husherehekewa duniani na wanawake kwa staili tofauti, wengine kwa kuandamana, kufanya makongamano, kutoa misaada mbalimbali na mambo mbali mbali yanayoendana na siku hiyo.
Matukio mbalimbali ikiwamo wanawake waliofanikiwa kutoa ushuhuda kwa wenzao walikotoka hadi kufikia walipo ili kutoa hamasa na wao waweze kufanya juhudi ya kufikia huko.
Katika baadhi ya ofisi, wanawake huwapumzisha wanaume katika uzalishaji na wao hushika usukani kuhakikisha kazi zinakwenda sawa bila kuwapo tofauti ya aina yoyote.
Hii imeongeza morari kwa wanawake na kujiona wanaweza kusimamia na kuendesha gurudumu bila kuonyesha upungufu.
Kwa miaka mingi wanawake wamekuwa wakililia usawa na mabadiliko yameanza kuonekana kutokana na kuwapo kwa nafasi za juu za viongozi kwa upande wao.
Nchi ya Tanzania kwa mfano imebarikiwa kuwa na Rais mwanamke ambaye tangu aliposhika madaraka hayo amefanya mambo makubwa na kuonyesha kuwa wanawake wanapokuwa viongozi hawashindwi.
Siku zote inaaminika kuwa mama ndiye kiongozi wa familia na kwamba akipewa nafasi ili mradi awe ana vigezo anaweza kuifanya kwa uadilifu.
Tangu alipoingia madarakani amefanya kazi kubwa ya kurudisha umoja na maridhiano ya kisiasa na wananchi wengi wamefurahia hatua hiyo na kumkubali.
Pia inasemekana kuwa sehemu yoyote ambayo mwanamke anaiongoza rushwa ya aina yoyote haina nafasi hata kama itakuwapo sio kwa kiwango kikubwa.
Juhudi za wanawake katika kusaka usawa zinachagizwa kupitia siku kama hii wanapokutana na kubadilishana uzoefu na mawazo, hivyo siku hii ni muhimu kwa wanawake wote kwa kuwa huwabadilisha kifikra na kimtazamo.
Ni muhimu pia wanawake wanapopata nafasi wakumbuke kuwashika mkono na wenzao kwa kuwapa mbinu, maarifa ili na wao waweze kufikia hatua walizofikia wenzao.
Kuna ile dhana iliyojengeka kuwa adui wa mwanamke ni mwanamke mwenzake, hii inaweza kuondolewa kwa kuonyesha kwa vitendo kwamba sio ya kweli kwa sababu wanawake wengi wamesaidiana na kunyanyuana iwe kibiashara au kwenye kazi za ofisini na hata kwenye masomo.
Mara nyingi wanaosambaza imani potofu ni wale ambao hawapendi kujishughulisha na kuwa na bidii ya kujiendeleza ili kufikia ngazi walizofikia wenzao na kubaki kulalamika na kuzua mambo yasiyo na ukweli.
Siku ya Wanawake Duniani kwa mara wa kwanza ilisherehekewa mwaka wa 1911 kutoka mataifa 11 duniani ambayo yalikusanya wanawake 100 walioanza kuiadhimisha siku hiyo.
Mwaka 1908 wanawake 15,000 waliandamana katika mji wa New York, nchini Marekani wakidai kupunguziwa muda wa kufanya kazi, kupata ujira wa kuridhisha na kupewa haki ya kupiga kura.
Mwaka 1909 mwanamke kwa jina la Clara Zetkin alipendekeza kuanzishwa kwa siku ya wanawake duniani katika mkutano wa wafanyakazi wanawake uliofanyika katika jiji la Copenhagen, nchini Denmark.
Baada ya mkutano wa wanawake Beijing nchini China, haki mbalimbali wanazostahili kuzipata zimeanza kutekelezwa.
**Hongera wanawake wote kwa kuadhimisha siku hii muhimu kwao.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Grace Gurisha

# Walimu kinamama acheni kuwatesa hawa wanafunzi

**LEO** kinamama ni 'vidole juu na vigelegele' tunasherehekea Siku ya Mwanamke Duniani, sote kwetu ni hongera.

Lakini, nikiangalia hili linaniumiza, walimu kinamama shuleni inasikitisha kumuona mwanafunzi muda wa masomo na wa mapumziko yupo barabarani ametumwa chai au chips ama mishikaki na mwalimu hasa kinamama.

Anampa kazi bila kujali kwamba anatakiwa kupumzika, kucheza na kusoma. Ni tabia ya walimu wengi wanawake na nimeshuhudia kwa baadhi ya shule ikiwamo Shule ya Msingi Kisutu Dar es Salaam.

Niwaambie mnautumia vibaya ualimu wenu kwa kuwatuma chai na vyakula wanafunzi muda wa darasani, wa mapumziko na kuwachosha.

Nimekutana mara kadhaa na baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo katika mgahawa wa jirani jina tunalo hapo Kisutu, ambao haupo mbali na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE).

Kwa kweli inasikitisha mzazi anajua mtoto anasoma kumbe yupo barabarani, akipata ajali, mwalimu anatoa maelezo gani?

Halafu ukiangalia kuna umbali kutoka shuleni hadi kwenye mgahawa huo, mwanafunzi akiwa barabarani anapishana na vyombo vingi vya moto magari, pikipiki na bajaji, hilo hamlioni?

Walimu tena kinamama hali hiyo ni hatari sana kwa usalama wa mwanafunzi kwa sababu asilimia kubwa ni wadogo na pia hakuna utaratibu wa mwalimu kumtuma mtoto nje ya shule tena kwa sababu zake binafsi, hasa kumnunulia chakula.

Kuna siku mwanafunzi katumwa chai ya maziwa, chips za shilingi 1,000 na mishikaki miwili saa 2:45 asubuhi, muuzaji akamwambia mishikaki bado kwa hiyo akae kwenye kiti asubirie aiweke jikoni.

Kwa kweli nilijikuta namtafakari huyo mwalimu aliyemtuma, kwa sababu ni muda wa darasani lakini mwanafunzi amekalishwa kitini anasubiri shibe ya mwalimu hii sio haki wala sawa, jitahidini kubadilika acheni wanafunzi wasome. Ni vyema pia serikali ikalisemea hili.

Kama imeliona la watoto wadogo kuwekwa bwenini hili nalo liangaliwe.

Nilijaribu kuwauliza kwa nini wanakubali kutumwa na walimu wakati wao wanatakiwa kuwepo shule, walidai kwamba wanashindwa kukataa kwa sababu wanaogopa kuchapwa na pia wataonekana ni wajeuri na hawana adabu.

Pia, wanadai kuwa ni wadogo hawawezi kuwakatalia walimu wao, kwa hiyo wanakubali tu kutumwa, walimu acheni kuwatesa watoto kwanza jua ni kali sana na pia ni usumbufu , kuweni mama, walimu na walezi pia.

Jifikirieni nyie walimu mtajisikiaje kama ungekutana na mwanao barabarani akiwa amebeba kichupa cha chai, bahasha ya mandazi , mishikaki chips muda wa masomo au wa mapumziko? Halafu anakueleza kwamba ametumwa na mwalimu, pengine ungerudi kupigana na kugombana walimu shuleni.

Kumbuka usifanye ambayo hupendi au hampendi ninyi kufanyiwa acheni kuwafanya wanafunzi wenu kama watumwa, wazazi na walezi wamewaamini ndiyo maana wakawakabidhi watoto wakiamini ninyi ni mikono salama.

Shule ina uzio, sasa cha kujiuliza hawa wanafunzi wanatokaje nje, kwa hiyo katika lango la kuingilia na kutoka hakuna walinzi? Kwa sababu hii inaonyesha usalama kwa wanafunzi ni mdogo mno.

Pia, picha hii inaonyesha dhahiri jinsi gani wazazi na walezi hawazungumzi na watoto wao kwa sababu kama wangekuwa wanazungumza basi kitendo hicho kisingeendelea kwa sababu hakuna mzazi au mlezi angependa mwanafunzi afanyiwe hivyo.

Wazazi amkeni na mfuatilie maendeleo ya watoto wenu inawezekana mtoto wako hafanyi vizuri masomo yake kumbe kwa sababu ni kibarua wa walimu kazi yake ni kutumwa hana muda wa kusoma wala kupumzika.

Hiki kinachofanyika ni unyanyasaji na ukatili kwa watoto halafu wengi wanaotumwa ni mabinti. Wazazi na walezi zungumzeni na watoto wenu inawezekana kuna mambo wanafanyiwa nyie hamjui.

## SIKU YA WANAWAKE DUNIANI



# HONGERA WANAWAKE THE GUARDIAN



Beatrice Shayo
**Mwandishi**



Romana Mallya
**Mwandishi Mwandamizi**

**MHARIRI MTENDAJI**



**Beatrice Bandawe**



Salome Kitomari
**Mhariri wa Habari**



Felister Peter
**Mhariri wa Habari**



Somoe Ng'itu
**Mhariri wa Michezo**




Gaudensia Mngumi
**Mhariri wa Makala**




Anjela Mhando — **Mwandishi**
Augusta Njoji — **Mwandishi**
Beatrice Moses — **Mwandishi**
Beatrice Philemon — **Mwandishi**
Christina Haule — **Mwandishi**
Latifa Mzungu — **Msanifu Lugha**
Dotto Charles — **Mwandishi mtandao**




Mwanabinti Aluwi — **Msanifu kurasa**
Christina Mwakangale — **Mwandishi**
Cynthia Mwilolezi — **Mwandishi**
Elizabeth John — **Mwandishi**
Elizabeth Zaya — **Mwandishi**
Getrude Mbago — **Mwandishi**
Mariam Mkanaka — **Mwandishi mtandao**



Getrude Mpezya — **Mpigapicha**
Grace Gurisha — **Mwandishi**
Grace Mwakalinga — **Mwandishi**
Hamida Kamchalla — **Mwandishi**
Idda Mushi — **Mwandishi**
Jenifer Gilla — **Mwandishi**
Mary Kadoke — **Mwandishi mtandao**



Julieth Mkireri — **Mwandishi**
Kulwa Mzee — **Mwandishi**
Mary Mosha — **Mwandishi**
Neema Sawaka — **Mwandishi**
Rahma Suleiman — **Mwandishi**
Renather Msungu — **Mwandishi**
Khadija Ngururu — **Mkutubi**



Bahati Hoza — **Mhariri Msanifu**
Zanura Mollel — **Mwandishi**
Woinde Shizza — **Mwandishi**
Tumaini Mafie — **Mwandishi**
Saada Akida — **Mwandishi michezo**
Restituta James — **Mwandishi**
Chiku Mbonde — **Ofisa madai**



Dorcus Sembuli — **Ofisa Matangazo**
Nailah Mhuyuka — **Mhasibu**
Rahma Ally Salum — **Mhasibu**
Rehema Shedrack — **Utawala**
Blandina Buluda — **Katibu Muhtasi**
Alice Michael Nyungi — **Ofisa Matangazo**
Merina Chahali — **Ofisa Matangazo**

# Waziri ageukia miji endelevu vijijini

**Munir Shemweta,** GEITA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amezitaka halmashauri nchini kuviandaa vijiji kuwa miji endelevu ya baadaye na yenye tija kiuchumi na kijamii kwa vizazi vijavyo.

Katika kufanikisha hilo, amehimiza upangaji wa vijiji na ujenzi wa nyumba kwa kuzingatia mwongozo wa upangaji na ujenzi wa nyumba bora vijijini.

Dk. Mabula amesema hayo jana wakati wa kikao kazi cha kujadili na kuweka mikakati ya kukwamua changamoto za urasimishaji makazi na sekta ya ardhi kwa ujumla katika mkoa wa Geita.

Alisema changamoto kubwa inayoikabili nchi kwa sasa ni kasi kubwa ya ukuaji vitovu vya vijiji inayoambatana na vijiji, hivyo kuendelea kupoteza hadhi ya kuwa vijiji kwa kusongwa au kumezwa na tabia za kijamii kwa ukuaji usio endelevu. Kwa mujibu wa Dk. Mabula, hali hiyo inatokana na usimamizi na utaratibu duni wa upangaji makazi na ujenzi wa nyumba bora vijijini katika hatua ya awali ya ukuaji.

Alibainisha kuwa upangaji ardhi ya vitovu vya vijiji na miji kwa ujumla ni mwanya mzuri wa kukuza fursa za uwekezaji na kuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo kwa wote huku watu wa kipato cha chini wakinufaika kupitia fursa za kibiashara zitokanazo na uhamiaji na ukaribu kati ya miji midogo na vijiji.

"Tanzania kwa sasa ina vijiji 12,318 kati ya hivyo zaidi ya vijiji 10,000 sawa na asilimia 80 vyote vimepimwa mipaka yake na kupewa vyeti vya ardhi vya vijiji na kati ya vijiji hivyo, vijiji vyenye mpango ya jumla ya matumizi ya ardhi ni 2, 675 sawa na asilimia 21.7 ya vijiji vyote," alisema.

Pia Waziri Mabula alisema vitovu vya makazi ya vijiji vingi nchini bado havijaandaliwa mipango kina ya kusimamia na kudhibiti shughuli za ukuaji kiuchumi na kijamii, hivyo kusababisha kuwapo changamoto ya ukuaji usio endelevu wa vijiji kama miji tarajiwa ya baadaye.

Alisema jambo hilo linatokana na mamlaka za upangaji kukosa kipaumbele katika kuzijengea uwezo serikali za vijiji ili kutimiza jukumu hilo la kuandaa mipango kina ya makazi ili kusimamia ukuaji wake kama miji ya baadaye.

Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeandaa Mwongozo wa Upangaji Makazi na Ujenzi wa Nyumba Vijijini mwongozo wenye lengo la kuwasaidia wakijiji kupanga makazi ya vijiji vyao na kujenga nyumba bora na za gharama nafuu kwa njia shirikishi kati ya wataalamu wa Mipangomiji, wanavijiji na wadau mbalimbali.




Mkurugenzi wa Kituo cha Maunga Orphanage, Zainabu Maunga, akiongea na waandishi wa habari wakati wa makabidhiano ya msaada wa chakula na mahitaji muhimu kutoka kampuni ya Mawasiliano ya Halotel Tanzania, Kinondoni jijini Dar es Salaam. Wengine ni Ofisa wa Huduma kwa wateja kutoka Halotel, Hanh Hong Thi Nguyen na baadhi ya watoto wanaolelewa kituoni hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WMA yapewa heko kuhusu vipimo bidhaa

**Na Joseph Mwendapole**

KAMATI ya Kilimo, Biashara na Utalii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, imeipongeza Wakala wa Vipimo (WMA) kwa kuhakikisha mwananchi anapata bidhaa kwa vipimo sahihi kulingana na thamani ya fedha anayotoa bila kupunjwa.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Yusuph Hassan Iddi, baada ya kamati hiyo kufanya ziara ya kujifunza kwenye kituo cha uhakiki cha WMA kilichoko Misugusugu mkoani Pwani.

Alisema kupitia ziara hiyo wamejifunza mambo mengi kwa kuwa na wao upande wa Zanzibar wana taasisi kama hiyo ambayo inaitwa Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA).

Alisema kuna mengi ya kujifunza kutoka WMA kutokana na ukongwe wake ili kuishauri Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuiwezesha taasisi yake ya ZAWEMA katika kusimamia usahihi wa vipimo kwenye maeneo mbalimbali.

Yusuph alisema taasisi hizo za vipimo ni muhimu kwa kuwa zinahakikisha zinamlinda mtumiaji wa mwisho wa bidhaa kupata vipimo sahihi ndiyo maana hata kwenye sekta ya afya mgonjwa anapimwa kwanza uzito ili apate dozi inayoendana na uzito wake kwa kuwa kinyume cha hapo anaweza kupata madhara.

Alisema kamati inaipongeza serikali kwa kuiwezesha WMA kujenga kituo kikubwa na cha kisasa ambacho kinafanya shughuli za upimaji wa matangi ya malori ya kusafirisha mafuta, lakini pia wameona mitambo ya kisasa ambayo inatumika kupima mita za maji na umeme kabla hazijaenda kufungwa kwa wateja.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, upimaji huo utasaidia kupunguza malalamiko kwa wananchi wanaotumia huduma hizo ndio maana kama kamati itashauri ili na upande wa Zanzibar waweze kupata kituo cha aina hiyo ili kuwalinda watumiaji wa huduma hizo.

Naibu Waziri Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliishukuru na kuipongeza kamati kwa kutembelea WMA katika kituo chake cha upimaji Misugusugu kwa ziara ya kujifunza kazi zinazofanywa na taasisi hiyo.

Kigahe alisema wajumbe wa kamati hiyo walitembezwa na kushuhudia kazi mbalimbali zinavyofanyika ikiwa ni pamoja na upimaji wa matangi ya malori ya kusafirisha mafuta, upimaji wa mita za umeme pamoja na dira za maji.

Alisema kupitia ziara hiyo anaamini wamejifunza mambo mengi lakini pia ni fursa ya kubadilishana mawazo ya namna ya kuboresha taasisi hizi na wamepokea ushauri uliotolewa na Kamati hasa kwenye eneo la kuweka alama kwenye dip stick kutumika njia za kisasa zaidi kuliko zinazotumika kwa sasa.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stela Kahwa, alisema ushirikiano baina ya ZAWEMA na WMA umeanza muda kwa kubadilishana uwezo wa kitaalamu na vitendea kazi ili kuhakikisha Wananchi wanapata bidhaa zenye vipimo sahihi.

Pia alisema taasisi hizo zinashirikiana kutoa elimu kwenye maonesho mbalimbali kama ya Mapinduzi na elimu ya vipimo kwa Wafanyabiashara mbalimbali kama masonara wanaouza vito na madini.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa ZAWEMA, Mohamed Simai, aliishukuru Kamati hiyo kwa kutenga muda kuja kujifunza namna shughuli za vipimo zinavyofanyika kwa kuwa anaamini itawasaidia kuishauri serikali ya Zanzibar kuiwezesha taasisi hiyo ili kupanua wigo wa utekelezaji wa majukumu yake na kuhakikisha inawalinda Wananchi katika sekta mbalimbali kwa kusimamia matumizi ya vipimo sahihi.

# Kituo watoto yatima chapata msaada Siku ya Wanawake

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Halotel, imeadhimisha Siku ya Mwanamke Duniani kwa kukabidhi misaada kwenye kituo cha kulelea watoto yatima cha Maunga mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa kukabidhi misaada hiyo, Ofisa Huduma kwa Wateja wa Halotel, Hanh Thi Nguyen, alisema miongoni mwa misaada iliyokabidhiwa ni kilo 670 za mchele, kilo 50 za maharage, lita 80 za mafuta ya kupikia, kilo 140 za unga wa mahindi na kilo 20 za sukari.

Misaada mingine alisema ni sabuni za kusafishia za kufulia, pakiti sita za taulo za kike na vifaa vingine vya kutumia katika kituo hicho ikiwamo nguo.

"Tumeona tutoe misaada hii kama zawadi kwa watoto hawa ili kuwaonyesha upendo na tunaamini kwa kufanya hivi itaongeza tabasamu kwao na watajiona kwamba wanathaminiwa na kupendwa na wengine,"alisema Hanh.

"Kwa kusaidia jamii ya Tanzania, ni miongoni mwa programu ya kurudisha kwa jamii katika kuboresha na kuwaletea tabasamu watu wanaoishi katika hali ngumu, kupitia utekelezaji wa majukumu ya Jamii ya Kampuni."

Alisema msaada huo ni sehemu ya ahadi endelevu ya kampuni hiyo ya kusaidia jamii ya Watanzania hususani wanaoishi katika mazingira magumu.

"Na hiyo ni sadaka ya kampuni ya kuonyesha upendo na huduma kwa jamii yenye uhitaji katika kuelekea siku muhimu ya kilele cha Siku ya Wanawake Duniani. Kama kampuni, tunatambua jukumu kubwa wanalolibeba wanawake katika jamii na uchumi. Tunafikiri ni jukumu letu sote kusaidiana nao kulitekeleza hususani walio na mzigo mzito wa malezi."

Hanh alisema kituo hicho kinalea na kusomesha watoto zaidi ya 120 ambao wamepoteza wazazi wao.

Hanh alisema mbali na msaada huo, pia katika maduka ya kampuni hiyo, wameandaa matukio mbalimbali ya kuongeza uelewa wa umuhimu wa usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake na kuomba wananchi kwenda kujifunza.

Alisema katika kusherehekea siku hiyo ya mwanamke duniani, Halotel imeandaa zawadi kwa mteja yeyote mwanamke ambaye atatembelea maduka ya kampuni hiyo kwa ajili ya kupata huduma yoyote.

"Mwanamke atakayetutembelea atakuwa na nafasi ya kupokea zawadi mbalimbali ikiwa ni pamoja na mavazi ya kiafrika, vocha na zinginezo, zote zimeandaliwa ili kuhamasisha na kuwezesha wanawake kwa uvumbuzi na teknolojia kwa ajili ya usawa wa kijinsia,"alisema Hanh.

Mkurugenzi wa kituo hicho cha kulelea watoto yatima, Zainab Maunga aliishukuru kampuni hiyo na kuomba wengine kuiga mfano wao.

"Tunathamini sana jitihada na msaada huu ambao tumeupokea kutoka Halotel wa kusaidia jamii na kituo chetu, tunaomba waendelee kuwa na moyo huo huo ili kuboresha maisha ya watanzania. Mchango wao kwa kituo chetu ni mfano wa dhamira waliyonayo kwa jamii ya Watanzania."



# Mil.380/- kujenga, kukarabati bwawa la maji Kwamizi

**Na Mwandishi Wetu,**
TANGA

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL), imewekeza Sh.milioni 380 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa bwawa la maji la Kwamizi lililoko wilayani Handeni mkoani Tanga.

Uwekezaji huo ni kutatua tatizo la ukosefu wa maji na kutoa huduma za majisafi na salama kwa Watanzania.

Mkurugenzi wa Uhusiano wa SBL, John Wanyacha, alisema uwekezaji katika mradi huo ni miongoni mwa miradi zaidi ya 20 ya maji ambayo imetekelezwa katika mikoa mbalimbali chini ya udhamini wa SBL kwa kushirikiana na Shirika la Water Aid.

"Chini ya programu yetu ya 'mpango wa maisha', tumekuwa tukitekeleza miradi ya maji katika mikoa kadhaa ili kuhakikisha upatikanaji wa majisafi na salama kwa jamii, safari hii tunaenda kuacha alama Handeni kwa mradi huu utakapokamilika," alisema.

Alisema baada ya kukamilika kwa mradi huo SBL inajipanga kuwashirikisha wananchi wa Handeni ambao watanufaika na mradi wa maji kuanza kilimo cha shayiri na kuuzia SBL kwa bei ya ushindani.

Wanyacha alisema mradi huo unaotekelezwa kwa ushirikiano wa Shirika la Water Aid na serikali ya mtaa wilayani humo, ulianza Februari 28 mwaka huu na unatarajiwa kukamilika Aprili 2023.

Alisema mradi huo unatarajiwa kuleta afueni kwa maelfu ya wakazi wa wilaya hiyo kufuatia uharibifu wa mabwawa na hivyo kusababisha jamii kukosa majisafi na salama.

Akizungumza katika ziara ya kutembelea mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Albert Msando alisema utaratibu wa ushirikiano kati ya serikali, SBL na Water Aid utakuwa na tija katika usimamizi wa muda na kiwango.

Hivyo aliahidi kuhakikisha usimamizi na utekelezaji mzuri wa mradi huo pamoja na msaada kutoka ofisi yake.

Mkurugenzi wa Uhusiano wa Kampuni ya East Africa Breweries Limited (EABL) ambayo ni kampuni tanzu ya SBL, Eric Kiniti alisema ana matumaini kuwa mradi huo utafanikiwa na utekelezaji wake utakwenda kama ilivyopangwa.




Mkurugenzi wa Fedha na Mipango wa Benki ya Azania, Jacqueline Lyatuu (wa pili kulia), akitoa mada katika mkutano wa pili wa wanawake na vijana wafanyabiashara barani Afrika, ulioandaliwa na Mtandao wa Uwezeshaji Wanawake Tanzania (TAWEN), uliomalizika jijini Arusha jana, ambapo benki hiyo ilikuwa mdhamini mkuu wa mkutano huo. Wengine ni Meneja Msaidizi wa TRA Arusha, Mathew Ruangisa (kulia), Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano UTT-AMIS, Daudi Mbaga (kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi ya CPB, Salim Awadh. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake KKKT Arusha wakemea vitendo vya ukatili

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

WANAWAKE wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jimbo la Arusha Mashariki Dayosisi ya Kaskazini Kati, wameadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa kukemea vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Akizungumza jana wilayani Arumeru, Mwenyekiti wa Wanawake KKKT Jimbo la Arusha Mashariki, Nembris Samwel, alisema kwa sasa matukio ya ukatili wa kijinsia yameshamiri duniani hasa kwa watoto na wanawake.

"Katika maadhimisho haya sisi wanawake tunapaswa kuungana kukemea matukio haya na kuelimisha jamii, jinsi ya kuondokana na ukatili na unyanyasaji wa kijinsia na sisi wanawake ndio walezi wa familia," alisema.

Kwa mujibu wa Nembris, wanawake ndiyo walezi wa familia kuanzia ngazi ya kulea watoto kiakili, hivyo hakuna budi kila mmoja akasimama kuhakikisha wanapinga matukio hayo.

Mwenyekiti Idara ya Wanawake kanisani hapo, Narivi Kyamba, alisema mwanamke akisimama katika jamii taifa litasimama kiuchumi, kijamii na nyanja zote za uongozi.

"Wanawake ni jeshi kubwa linaweza kuleta mabadiliko katika kutokomeza ukatii na unyanyasaji katika jamii, lakini hili linawezekana kama kila mmoja akisimama katika nafasi yake," alisema.

## Aadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa kuwapeleka watoto hifadhi ya taifa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

BALOZI wa utalii nchini, Isabella Mwampamba, ameadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kwa kuwapeleka katika Hifadhi ya Taifa Ruaha, watoto watatu wenye ulemavu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Isabella alisema lengo la kuwapeleka watoto hao katika mbuga hiyo iliyopo mkoani Iringa ni waende kujionea vivutio lukuki vilivyopo wakiwamo wanyama.

Isabella alisema ameamua kutumia maadhimisho hayo kumkumbuka mwanamke anayeteseka kwa miaka 50 akilea watoto wake watatu ambao ni walemavu.

Alisema watoto hao pamoja na mama yao wamekuwa wakiishi bila kupata fursa hata ya kutembelea vivutio vilivyoko nchini, kutokana na hali duni ya maisha waliyonayo.

Alisema kabla ya kuwapeleka hifadhini alifanya jitihada mwaka jana, kuonana na Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa ili kuisaidia familia hiyo.

"Nashukuru sana Waziri Majaliwa alitoa Shilingi milioni tano na tumejenga nyumba nzuri na wiki hii ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani tumeizindua, lakini na mimi kupitia wadau mbalimbali tupo katika jitihada za kuwapelekea maji na umeme," alisema.


Alisema baada ya kuwafikisha hifadhini wamefanikiwa kuona wanyama wakiwamo simba, nyati, tembo, swala na wengine wengi.

Hivyo, aliwaomba wadau kusaidia familia hiyo kwani mama mzazi amezeeka kwa sasa na nguvu ya kumudu kuwabeba na kuwaogesha inaisha.

Wakizungumza na waandishi wa habari, watoto hao Eliasi na Jenifer walimshukuru Waziri Majaliwa kwa kuwajengea nyumba na Isabella kuwapeleka katika hifadhi.

Mama mzazi wa watoto hao, Anjelista Kihanza, alishukuru kwa kupelekwa kutalii na watoto wake akisema kitendo hicho ni faraja kwake na kina thamani.

Pia alimshukuru Waziri Majaliwa kwa kuwasaidia kujengewa nyumba bora na kuwawezesha kuishi mazingira safi.





# Polisi yashikilia bunduki zilizotumika kwenye mauaji ya Katibu wa CCM

**Na Richard Makore,**
MWANZA

JESHI la Jeshi Polisi mkoani Kagera limesema linashikilia bunduki mbili za Kampuni ya Ulinzi ya Sammit zinazodaiwa kutumika katika mauaji ya Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Lespikius Asporo katika Kata ya Rutoro wilayani Muleba mkoani Kagera.

Limesema linawasaka walinzi wa kampuni hiyo ili kulisaidia Jeshi la Polisi kupata ukweli wa tukio hilo ambalo lilitokea hivi karibuni katika ranchi ya mifugo ya Kagoma ambayo inamilikiwa na mwekezaji.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Mateti Msangi, alisema walinzi wa kampuni hiyo wanadaiwa kumpiga risasi katibu huyo wa CCM na kupoteza maisha.

Alisema siku ya tukio wananchi wa eneo hilo akiwamo katibu huyo waliingia eneo la ranchi hiyo ya mifugo wakiwa na silaha za jadi hatua ambayo iliwafanya walinzi wa kampuni hiyo kujihami.

Kamanda Msangi alisema katika purukushani hizo katibu huyo wa CCM alipigwa risasi.

Alifafanua kuwa tukio hilo lilitokea Machi 1, mwaka huu na polisi walianza msako wa kuwanasa watuhumiwa usiku wa siku hiyo hiyo.

Kamanda Msangi alisema eneo hilo la mwekezaji lina vitalu vingi vya kufugia mifugo na kwamba analimiki kihalali kwa kufuata sheria zote.

Aliongeza kuwa baada ya tukio hilo walinzi hao walitoroka na kutokomea kusikojulikana na kwamba polisi wanaendelea kuwasaka ili wafikishwe katika vyombo vya sheria.

Akitoa historia ya mgogoro huo, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Charles Mwijage, alisema Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) iligawa vitalu vya ufugaji kwa wawekezaji kwa kuwapatia maeneo ambayo tayari kulikuwa na vijiji.

Mwijage akizungumzia mgogoro huo bungeni alisema ulianza tangu mwaka 2005 na kuanzia hapo kamati nyingi ziliundwa ili kutatua tatizo hilo.



Kaimu Naibu Mrajisi (Uratibu na Uhamasishaji) wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Consolata Kiluma (kushoto), akikabidhi tuzo kwa Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Hamis Majogoro, wakati wa Jukwaa la Maendeleo ya Ushirika, mkoani Shinyanga juzi, baada ya chama hicho, kufanya vizuri kwenye ushirika kuliko vyama vingine katika mkoa huo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Vyama vya ushirika 159 vyafutiwa usajili kisa uzembe

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

VYAMA vya ushirika 159 mkoani Shinyanga vimefutwa kutokana na kushindwa kufanya kazi vizuri, huku vingine 38 vikitarajiwa kufutwa na kuwa vituo vya kununulia pamba.

Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Shinyanga (COASCO), Hilda Boniphace, alibainisha hayo juzi wakati akisoma taarifa kwenye jukwaa la maendeleo ya ushirika mkoani Shinyanga, lililofanyika katika Chuo cha Ushirika Moshi tawi la Kizumbi katika Manispaa ya Shinyanga.

Alisema kwenye ushirika kumekuwapo na vyama vingi ambavyo havijafanyiwa kazi vizuri na hivyo ameamua kuvifuta na kwamba mwaka huu wameshafuta vyama 159.

Alisema katika mikakati ambayo wamejiwekea kwa msimu ujao ni kuhakikisha vyama vya ushirika zaidi ya 153 ambavyo vilipata hati mbaya vinapata hati safi kwa sababu wameshabaini upungufu wao ikiwamo kutofutiwa madeni ya nyuma.

Mkaguzi wa COASCO, Rodrick Kilemile, alisema katika ukaguzi ambao wameufanya mwaka 2021/2022 kwa vyama 237, vilivyopata hati safi ni saba, yenye mashaka 51, isiyoridhisha tatu na hati chafu 176.

Kaimu Naibu Mrajisi Uratibu na Uhamasishaji Tume ya Maendeleo na Ushirika Tanzania (TCDC), Consolata Kiluma, aliwataka viongozi wa vyama vya ushirika kuacha kufanya kazi kwa mazoea bali wafuate sheria za ushirika na kanuni zake.

Alisema vyama vingi vya ushirika vimekuwa vikifanya vibaya kutokana na viongozi wao kuwa wazembe.

# Wasiojulikana wavamia nyumba, wafanya ubakaji, wapora

**Elizabert Seleman,**
SENGEREMA

WATU wawili wanadaiwa kuvamia nyumba ya mkazi wa Kijiji cha Sima wilayani Sengerema mkoani Mwanza, Ester Deus (35), kumbaka kisha kuiba baadhi ya vitu ikiwamo nguo.

Tukio hilo lilitokea juzi usiku katika kijiji hicho wakati Ester akiwa nyumbani kwake amelala, huku mume wake akiwa kazini.

Akizunguma na waandishi wa habari, Ester alisema kuwa tukio hilo lilitokea majira saa nane usiku na kwamba alishtuka kutoka usingizini na alipotazama mlangoni aliona mwanga wa tochi ukimulika machoni, huku vijana wawili wakiwa wameshika visu na mapanga.

Alisema baada ya vijana hao kuingia ndani walimuaru avue nguo, wakaanza kumbaka.

Ester alisema kitendo alichofanyiwa na watu hao kimemfanya apoteze amani na kuingiwa na uoga hususani wakati wa usiku mume wake asipokuwapo.

Mume wa Ester, Masunga Ngaza alisema tukio hilo lilitokea wakati akiwa kazini.

Masunga aliomba serikali kuhakikisha sheria inafuata mkondo wake kwa watu waliombaka mke wake ili haki ipatikane.

Baadhi ya wananchi waliozungumzia tukio hilo, waliomba serikali kuwachukulia hatua kali za kisheria vijana hao waliofanya kitendo hicho ili liwe fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hiyo.

Mwenyekiti wa kitongoji cha Nyingumba, Patrick Kilinga, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo akisema ni la kwanza kutokea katika kitongoji hicho.

Alisema wananchi wa kitongoji hicho walifanikiwa kumkamata kijana mmoja kati ya hao wawili anayedaiwa kufanya tukio hilo na kumpeleka Kituo cha Polisi Sengerema.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, Wilbroad Mutafungwa, alipoulizwa kwa njia ya simu kuhusu tukio hilo alisema hajapata taarifa, lakini aliahidi kulifuatilia.



Ukurasa 12

**RC mwanamke anayethibitisha 'tunaweza' kwa vitendo kupitia anayofanikisha kazini**



Ukurasa 13

Miaka 15 iking'ara na makubwa Mfuko wa Wanawake - WFT-T

# Siku ya Wanawake Duniani

JUMATANO MACHI 8, 2023

Nipashe



Ukurasa 14

**Daktari aliyepata saratani ya matiti, asimulia siku alivyopokea vipimo**

SAMIA; RAIS WA MAFANIKIO NDANI NA NJE

# Kuingia kazini tu, akaanza kung'ara kitaifa na kimataita 'kazi ikaendelea'

- Bajeti ya tabasamu; akadhibiti UVIKO-19
- Siasa kaimudu, sifa yake 'mama hana shida'

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA ya Rais Samia Suluhu Hassan, imeng'ara mwaka huu akionyesha kuwa ni mwanamke na kiongozi wa shoka nyumbani Tanzania na barani Afrika.

Anaanza kuvuta hisia za Waafrika pale anapokabidhiwa jukumu la kuuongoza ujumbe wa pamoja wa Afrika katika mkutano wa jukwaa la uchumi na biashara duniani (WEF) huko Davos Uswizi.

Ni tukio la Januari mwaka huu lililowaleta pamoja wakuu wa nchi, viongozi wa serikali kutoka mataifa mbalimbali na Afrika ikiwa ina sehemu yake.

Hata hivyo, changamoto za umeme zilimkwamisha Ramaphosa na Mama Samia akaiongoza Afrika.





Rais akiwasilisha ya Waafrika huko Davos, Januari mwaka huu. **PICHA: IKULU**

### KWANINI KUKUBALIKA?

Rais Samia anakubalika kimataifa kutokana na mwelekeo wake ndani na nje mipaka ya Tanzania. Tangu kuchukua jukumu la kuliongoza taifa, ametaka maridhiano na uhimilivu wa kisiasa akiondoa katazo au zuio la miaka saba kwa vyama vya upinzani kuwa na hadhara za kisiasa na kuendesha mikutano yoyote kwa maelezo kuwa kinachohitajika ni kuchapakazi.

Kuanzia mwanzoni mwa mwaka huu ameviruhusu kufanya mikutano na kuendelea na hadhara za kisiasa zilizokuwa zimezuiliwa na uongozi wa John Magufuli.

Rais Samia amefanikisha kuwapo kwa utulivu katika siasa nchini na kutekelezwa kwa maridhiano hayo kumeonekana, mosi, mara kwa mara anakutana na viongozi wa vyama vya siasa, anasikiliza na kufanyia kazi masuala yao.

Anataka utulivu wa kisiasa kama kupitia sheria zinazolalamikiwa kwenye uchaguzi, ameunda kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, akilenga muda wote kuwa na uongozi na kufanyakazi kwa uwazi.

### MTANGAMANO EAC

Rais Samia ni sura ya Afrika, baada ya kuanza kuongoza nchi, alifanya ziara nchini Kenya na amekuwa mstari wa mbele kutaka kuimarishwa biashara baina ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Akiwa Nairobi ameshiriki kuondoa vizuizi vya kibiashara na nchi za Afrika Mashariki na anakubaliana na viongozi wenzake kuhusu kuwa na Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) na Tanzania kuwa mshiriki anayeuza bidhaa na huduma.

Itakumbukwa kuwa Machi 2018 Umoja wa Afrika ulikubaliana na kutia saini mkataba wa makubaliano ya kuwa na AfCFTA, jukumu lililofanyika jijini Kigali Rwanda.

Rais Samia, anasimamia na anaunga mkono kuwapo kwa Soko Huria la Afrika na anataka ushiriki wa Tanzania katika soko hilo mambo yanayozidi kumpa sifa za kuongoza ujumbe wa Afrika Davos. Inapozungumzwa Afrika, sura halisi ya bara hilo inaweza isionekane kikamilifu iwapo Rais Samia hataonekana.

### KUINYANYUA TANZANIA

Rais Samia amekuwa shujaa kwenye matumizi ya fedha za UVIKO-19, ambazo ni zaidi ya Shilingi trilioni moja zilizotolewa na IMF kukabiliana na janga la Corona.

Hakufanya ajizi Tanzania ilizipokea na kufanya uwekezaji mkubwa si wa kununua vitakasa mikono, wala barakoa kama anavyoeleza Balozi Pindi Chana, akizungumzia uwekezaji kwenye utalii, badala yake amezifanyia kazi kubwa.

Ni pamoja na kujenga miundombinu na kutoa huduma zinazoonekana kuanzia madarasa mapya ya msingi na sekondari, kadhalika kuongeza vituo vya afya, ujenzi wa hospitali zanye vifaa tiba na huduma za kisasa.

Aidha, kuboresha sekta karibu zote ikiwamo ya utalii kwa kutumia fedha hizo za kusaidia Afrika kutatua changamoto za kiuchumi zinazosababishwa UVIKO-19 na athari za vita vya Ukraine na Urusi.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu watalii wa kigeni 1,175,697 walitembelea Tanzania kati ya Januari na Oktoba mwaka 2022, ikilinganishwa na watalii 716,741 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Watalii waliongezeka ni 458,956 sawa na ongezeko la asilimia 64 sababu kubwa ikiwa ni juhudi za kuendeleza utalii baada ya kuathiriwa na janga la UVIKO-19 na vita.

### KUKATAA UHASAMA

Rais Samia anagusa mioyo ya Watanzania kwa kuondoa migogoro na uhasama iliyosababisha wanasiasa Tundu Lissu, Makamu Mwenyekiti CHADEMA Bara kuishi uhamishoni.

Aidha, uhasama umemalizika na sasa Lissu amerejea nyumbani, huko wana CHADEMA wakishuhudia mbunge wa zamani wa Arusha Mjini, Godbless Lema, akirudi nyumbani kwa amani kutoka uhamishoni Canada.

Halikadhalika, Lema amefutiwa kesi zilizokuwa zinamkabili na sasa yuko huru kunguruma majukwaani kuendeleza haraka za demokrasia ya vyama vingi.

Wanawake wanaposherehekea siku yao leo wana kila sababu ya kusisitiza mshikamano na serikali ili kazi bora iendelee.

MWANAMVUA MRINDOKO

# RC mwanamke anayethibitisha ‘tunaweza’ kwa vitendo Katavi

**Na Neema Hussein, MPANDA**

JINA lake ni Mwanamvua Hoza Mrindoko, mwanamama Mkuu wa Mkoa Katavi. Katika mazungumzo yake maalum na gazeti Nipashe, wiki hii ofisini kwake mjini hapa, anatamka kuipokea Siku ya Wanawake Duniani, kwa mtazamo chanya na matarajio makubwa kuwasaidia kinamama wote duniani.

Hapo Mrindoko anamwaga busara zake kwao za kujitambua, kujielewa, kujikubali na kujithamini kuwa ni nguzo muhimu ya kuleta mabadiliko chanya kwa jamii.

Kwa mwanamke wa Katavi, anasema ni kujivunia ni fursa zao za kiuchumi kimkoa, kilimo cha mazao kama mpunga, mahindi, alizeti, korosho, tumbaku, karanga, maharage na mboga, ikiendana na fursa za uchakataji wa mazao kwa mashine na kuwekeza katika ufungashaji mazao hayo, pia biashara zake.

Mrindoko anahamia kwenye mifugo, akianika fursa za ufugaji ng’ombe, mbuzi, kuku na masoko yake, akitaja mfano wa nchi jirani; Jamhuri ya Kidemokrasia Congo (DRC) na mwingiliano wa nchi za Burundi, Rwanda na Zambia, kupitia Ziwa Tanganyika na mkoa wa Kigoma, unaopakana nao.

Mengine anataja ni uchumi wa madini yanayopatikana ndani ya mkoa, akiwa na mifano ya dhahabu, shaba, ujenzi wa miamba kutengeneza kokoto, mchanga maalumu wa ujenzi na mawe ya ujenzi, vilevile akidokeza fursa za ajira kwenye miradi ya ujenzi katika sekta za afya na elimu.




Mkuu wa Mkoa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, akiwa ofisini kwake. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

### MAMA NA UONGOZI

Katika uongozi, Mrindoko anawatetea wanawake akitumia mfano binfasi, pia viongozi wengine kinamama mkoani Katavi akimtaja Mkuu wa Wilaya Mpanda, Jamila Yusuph na Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Sophia Kumbuli.

Wengine ni wakurugenzi watendaji: Teresia Irafai (Mlele) na Catherine Mashala (Mpimbwe).

Hapo anajumuisha juhudi zake na timu aliyoitaja, wanachangia kujipanga kuwafanya wanawake wa Katavi, wajitambue kuanzia ngazi ya familia, wakiwamo watoto, ili kuufanya mkoa na Taifa uwe na maadili mema, wakiwaonyesha fursa zilizopo ndani ya Katavi, wakiwasimamia na kuwapa maelekezo na mwelekeo sahihi.

Anautaja mradi wa Bandari ya Karema, ni wa kimkakati kwa mkoa, kwa vile umepakana na nchi jirani za DRC na Burundi, kupitia Ziwa Tanganyika na nchi ya Zambia, hali inayoifanya bandari hiyo kuwa fursa kubwa kiuchumi Katavi.

### SURA YA MAFANIKIO

Mrindoko anataja mafaniko mpaka sasa kimkoa, ni utekelezaji miradi ya serikali ya afya, kwa kupatikana hospitali ya rufani ya mkoa, hospitali za wilaya, vituo vya afya, zahanati, dawa na vifaa tiba. Pia kuna hatua kama hiyo kwenye elimu.

> “ Nimeagiza wakuu wa wilaya kuwasaka hao wanafunzi ambo ni asilimia saba ya wanafunzi waliobaki, sawa na wanafunzi takribani 1,400 watafutwe popote walipo, waende kwenye madarasa walizopangiwa.

Mafanikio mengine anayataja, ni kwenye utoaji mikopo kwa makundi ya wanawake, takribani asilimia 85 ya uwezeshaji mikopo unawaendea kinamama, akiwasifu wanaitumia vizuri, hali kadhalika wana mwitikio mkubwa kwenye makongamano ya mkoa ikilinganishwa na wanaume.

### CHANGAMOTO?

Mkuu wa Mkoa anataja changamoto kubwa anayoiona Katavi katika miaka miwili ya uongozi wake, ni mila na desturi zinamzuia kufikia ndoto au malengo yake. Anafafanua: “Zipo mila ambazo zinawazuia wanawake kusoma au kufikia mwisho wa masomo yao, ikiwamo kukatisha masomo kwa watoto wa kike na kutaka kuwaozesha...”

Anaendelea: “...Chagolaga’ hiyo ni mila ya kabila la Wasukuma waliomo mkoa wetu wa Katavi na kama unavyofahamu, kabila hilo tunao wengi ndani ya mkoa wa Katavi.

“Hiyo inaleta suala kama la unyanyasaji au kutokumpa nafasi mwanamke kuchagua mwenza anayempenda kwa dhati, badala yake mila ile inafanya mwanamke anachukuliwe na mwanaume ambaye hakutarajia anaweza kuwa mwenza wake.

“Jambo kama hilo husababisha wanawake wanakumbana na vipigo kwenye ndoa na unyanyasaji mwingine kuondoa sababu ikishatokea vile hapaswi kukataa akishachaguliwa kwenye zile ngoma za kiasili. Hiyo inatupa wakati mgumu kuwabadilisha wanawake, sababu hata tunapohitaji kuwafikia, inabidi tupite hatua ndefu...”

Anaeleza kuwa wanaendelea kutoa elimu kwa makundi ya kijamii kuwahamasisha, waone mwanamke anahitaji kupewa nafasi ya kusikilizwa na kufanya uamuzi wa yanayomuhusu, jamii yake na ashiriki kumiliki ardhi na mali, atoe mchango wake kwa jamii.

Mrindoko anataja halmashauri inayoongoza kwa mila hizo ni Mpimbwe, yenye mwingiliano mkubwa wa makabila. Hapo anakemea:”Nilipiga marufuku, nikawaagiza wakuu wa wilaya, wakurugenzi, maofisa maendeleo ya jamii na maofisa ustawi wa jamii, kuhakikisha wanatoa elimu ya kuachana na mila hiyo, sababu...”

### AFYA & ELIMU

Mrindoko anasema Katavi imepiga hatua katika suala la mama kujifungua kwenye vituo vya afya, ikilinganishwa na awali, wengi wakijifungulia majumbani na hata kukutwa na magumu ya kiafya, kwao na watoto.

Pia anakiri Katavi kukumbwa na maradhi surua, ukianzia na Halmashauri ya Wilaya Mpimbwe, kisha Tanganyika na baadaye Nsimbo na iko Mpanda na juhudi za tiba zinaendela, ikiwamo kutoa chanjo kwa watoto wote walio na umri chini ya miaka mitano.

Katika elimu, anataja sura ya ushindi, akisema mkoa unafanikiwa kwa uandikishaji watoto elimu ya msingi wakivuka malengo zaidi ya asilimia 100 kwa walioanza darasa la kwanza, elimu ya awali wamefikisha asilimia zaidi ya 90; na sekondari walioripoti shule ni takribani asilimia 93, kwa takwimu za hadi Machi 3, mwaka huu.

“Nimeagiza wakuu wa wilaya kuwasaka hao wanafunzi ambo ni asilimia saba ya wanafunzi waliobaki, sawa na wanafunzi takribani 1,400 watafutwe popote walipo, waende kwenye madarasa walizopangiwa,” anasema.

“Upande wa ufaulu, pia tunaendelea vizuri darasa la saba, kidato cha pili, kidato cha nne, kidato cha sita madarasa yote hayo hakuna darasa ambalo tuko chini ya asilimia 80 katika suala la ufaulu, tunahitaji kufanya kazi zaidi kuhakikisha tunazidi asilimia hiyo,” anasema.

“Suala la wanafunzi wanaofeli kidato cha pili na kukataa kurudia ni kweli lipo ndani ya mkoa wa Katavi, lakini tunafanya jitihada za kutoa elimu na kuhamasisha jamii na kuchukua hatua za kisheria, maana huo utakuwa ni utoro kama utoro mwingine.... tutachukua hatua kwa mwanafunzi mtoro,” anaagiza.

Anataja orodha vyuo mkoani ni: Ufundi VETA (Mpanda);Chuo cha Maendeleo ya Jamii Msaginya; Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo - Kampasi ya Mizengo Pinda; Chuo Kikuu Huria, Kampasi ya Katavi iliopo Mpanda; na Chuo cha Afya, akiwaombawakazi wa Katavi kutumia fursa hizo wakaongeze ujuzi na maarifa.

### HALI YA USALAMA

Mrindoko, anaanza kwa kushauri wazazi wenye vijana anaowaeleza ‘hawajui cha kufanya’ kuwapeleka katika vyuo vya ufundi kupata ujuzi na stadi, huku ikisaidia kupunguza tatizo la makundi ya kihalifu, yakiwamo yaliyowahi kujitokeza kwa majina kama: Damu chafu; Kaburi Moja na Manyigu.

Kwenye ukatili wa kijinsia, mama huyo anaanza kwa kukiri ni shida ndani ya mkoa, ikitendwa kwa wanawake na yanashughulikiwa na vyombo vya dola, ikiwamo polisi, hasa kupitia kitengo cha jinsia.

Anasema utafiti wa kiserikali kwenye halmashauri zote kupitia kamati za wilaya, wamebaini kuwapo ukatili, zaidi ni kujichukulia sheria mkononi, vipigo, manyanyaso, ubakaji, ulawiti wa watoto na hasa wanafunzi, ndoa za jinsia moja, yaani ushoga, vilevile ni tabia kama hiyo kwa dada zao.

Mrindoko anataja hatua wanazochukua ni kusimamia sheria kuhakikisha kunakotokea, wanachukua hatua kisheria, akinena: “Kupaza sauti kuanzia ngazi ya familia kama kuna dalili zozote za kufanyika kwa jambo hilo ndani ya familia, ihakikishe jambo hilo halifanyiki linazuiliwa na halitokei na kwenye ngazi ya jamii...

“Lingine tunalofanya ni kuhakikisha shule zetu za msingi na sekondari zinazingatia kanuni, taratibu na sheria ambazo zitahakikisha kwamba ukatili wa namna ile wanafunzi kwa wanafunzi kufanyiana vitendo nilivyotaja hauendelei kutokea.”

### HISTORIA YAKE

Mrindoko anasimuilia mwanzo wake, kwamba hakutarajia kikazi kufikia wadhifa wa sasa. Aliajiriwa akiwa mtumishi wa umma ngazi ya halmashauri, katika Ofisi ya Mkuu Mkoa Tanga na baadye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Tanga, kisha akahamishiwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Tanga (sasa jiji).

Mrindoko anasema, baadaye akakwea kupandishwa ngazi ya mkuu wa idara mbalimbali, ikiwamo, hata baadaye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri mbili ; Nachingwea na Kisarawe, kisha Mkuu wa Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma, hadi akakwea sasa Mkuu wa Mkoa wa Katavi.

# Miaka 15 iking'ara na makubwa Mfuko wa Wanawake - WFT-T

**Na Ananilea Nkya**

NI mfuko unaotoa ruzuku kwa ajili ya kuendesha utetezi wa haki za wanawake, wasichana na watoto nchini (Women Fund Tanzania-Trust-WFT-T), ukihesabu mafanikio makubwa tangu ulipoanzishwa miaka 15 iliyopita.

Kuna hatua ya kuwezesha mashirika ya utetezi yafanyayo kazi katika jamii, kuendesha shughuli zake, ambazo zimezaa matunda na kuacha alama muhimu inayoelimisha jamii kuhusu haki za wanawake, wasichana na watoto.

Mwenyekiti wa WFT-T, Prof. Ruth Meena, anasema mafanikio yamewezekana, akifafanua kwamba "ndani ya miaka 15 WFT-T, imejenga taasisi na mifumo imara, inayowezesha mfuko kukua na kuwa endelevu katika nyanja ya rasilimali watu na fedha, pamoja na ajenda yake ya kifeminia."

Anatoa mfano, katika muda mfupi, ruzuku za WFT-T ziliongezeka na sasa ni takribani asilimia 60 za ruzuku zikielekezwa ngazi ya jamii, kuwezesha vikundi vya wanawake kuendeleza vuguvugu la utetezi wa haki zao kiuchumi, kijamii na kisiasa, wakipinga yote yanayoendelea kuwabagua katika kufikia, kutumia na kunufaika na rasilimali za taifa.

Kwa mujibu wa Prof. Ruth ruzuku inayotolewa na WFT-T inawalenga watu wa kawaida na wasiofikiwa kutokana na mifumo ya ubaguzi kwenye utoaji ruzuku na kufikia rasilimali za taifa.

Mwenyekiti huyo, msomi wa sayansi ya siasa na utawala wa umma, anaendelea: "Masharti ya utoaji ruzuku ni rafiki na mfuko unawezesha walioonyesha dhamira na nia ya kuleta mabadiliko na wanapewa uwezo wa kutayarisha andiko.

Anafafanua: "Ruzuku zilizotolewa, zimeonyesha matokeo chanya kijamii na hata kitaifa."

Mafanikio ya WFT-T yaliwekwa wazi na wadau mbalimbali, kwenye maadhimisho ya miaka 15 yaliyofanyika Dar es Salaam, Februari mwaka huu.

Anataja mfano hai ni shirika la MUMITIE linalotetea haki za wanawake, wasichana na watoto katika ngazi ya jamii, huko Loliondo mkoani Arusha, likiwatetea na kutoa funzo kwa wanaume wanaotenda ukatili dhidi ya wanawake na wasichana, hata kuangukia mikasa ya jinai.

**VIONGOZI WANENA**

Akizungumza katika sherehe hizo za kuadhimisha miaka 15 ya WFT-T, Mkurugenzi Mtendaji wa MUMITIE, Rose Njiro, anasema shirika lake lilifanikiwa kuendesha kesi mahakamani, katika matukio mwanaume aliyeshirikiana na mwenzake kijinsia, kumpiga mke na kisha kumtupa porini katika mazingira ya kudhuriwa na wanyama. Hukumu ilipotoka, mshtakiwa akaangukia kifungo kirefu jela. Mkurugenzi Mtendaji wa MUMITIE, anasimulia mke huyo aliokolewa na wasamaria wema.

Shirika lingine linalofanya kazi ngazi ya jamii na lilipata ruzuku kwa nyakati tofauti kutoka WFT-T, imetoa matunda yanayoonekana ya Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), mkoani Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa WAJIKI, Janeth Mawiza, anasema wamekuwa wakiendesha kampeni 'nyumba kwa nyumba' kuipa jamii uelewa wa rushwa ngono inavyoathiri maendeleo yao kwa ujumla.

Anasema, ni kampeni inayowahusu wanafunzi, ikijulikana kwa jina 'Safari Salama Kwa Mtoto wa kike Bila Rushwa ya Ngono."

Mawinza anasema: "Kampeni hii imeanza kushika kasi mkoa wa Dar es Salaam, tumewafikia madereva wa pikipiki na makondakta wa daladala katika maeneo kadhaa ikiwepo Gongolamboto, Mbagala na Kinondoni."

Kwa mujibu wa Mawinza, ni kampeni inayochukua hadhi ya kipekee, ikiwezesha kufanyika utafiti wa rushwa ya ngono katika taasisi za vyuo vikuu na athari zake. Mwenyekiti wa WFT-T, Prof. Ruth Meena, anaeleza kuwa wahanga wa rushwa ya ngono walivunja ukimya, kwa kueleza ukweli wa matukio hayo na athari zake kwa wanafunzi wa kike.

Prof. Meena ambaye amefundisha katika vyuo vikuu, anaeleza:"Yamewezesha TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) kuendesha kampeni ya kitaifa ya kupambana na rushwa ya ngono katika sekta ya elimu."

> Ni kampeni inayowahusu wanafunzi, ikijulikana kwa jina 'Safari Salama Kwa Mtoto wa kike Bila Rushwa ya Ngono.

**UPEKEE WA MIFUKO**

Mwanzilishi Mwenza, Mkurugenzi Mtendaji wa kwanza wa WFT-T, Mary Rusimbi, anasema mifuko ya udhamini wa wanawake ni kitu kipya kilichobuniwa duniani miaka ya karibuni, kuwezesha ufadhili katika kazi za utetezi wa haki za wanawake, ndani ya zama za utandawazi.

Anaeleza ubunifu huo ulivyoanza na mfuko wa kimataifa, pia nafasi ya kumdhamini mwanamke, sasa duniani kote kumeshaanzishwa mifuko 44, katika mabara tofauti, ikiwamo WFT-T ya Tanzania.

Rusimbi anasema, mifuko ya udhamini wa wanawake, inaongozwa na mawazo na inaaminika kupatia ufadhili wa mashirika ya utetezi wa haki za wanawake, wasichana na watoto, ikitajwa ni njia sahihi ya kuleta usawa wa jamii na kutokomeza ukatili wanaofanyiwa mamilioni ya wanawake, wasichana na watoto duniani.

Kihistoria, WFT-T ilianzishwa kutokana na mahitaji ya wanawake na baada ya kufanyika utafiti wa mtandao wa jinsia mwaka 2008, ulionyesha hitaji kubwa la fedha za uendeshaji shughuli za utetezi wa haki za wanawake, wasichana na watoto katika ngazi zote.

Ngazi ya pili ya ruzuku za WFT-T, inaelekezwa kujenga nguvu za pamoja kwa mitandao na majukwaa ya mashirika ya wanawake, yanapounganishwa kufanya kampeni kitaifa kutetea haki za wanawake, wasichana na watoto.

Prof. Meena, mwanazuoni wa haki za binadamu, anasema WFT-T imewezesha kujenga na kuimarisha mitandao, majukwaa na kutoa utetezi wa haki za wanawake, wasichana na watoto, ikijenga vuguvugu la utetezi wa mabadiliko ya mifumo kandamizi katika sheria, sera, mipango na bajeti zisizo na mrengo wa kijinsia.

**NGAZI ZA MAFANIKIO**

Hapo anatoa mfano wa maeneo, Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi, kwa kuongozwa na Shirika la Msichana Initiative, iliendesha kesi katika Mahakama Kuu mwaka 2015, ilipobatilisha Kifungu cha 14 cha Sheria ya Ndoa ya Mwaka1971, kinachokinzana na haki kikatiba za mtoto wa kike.

Mahakama ya Rufani mwaka 2019, nayo ilikazia hukumu hiyo, baada ya pingamizi ya serikai kushindwa na sasa anasema, wanaendelea na kampeni ya kitaifa, kulishawishi Bunge lifanye marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

"Kwa kweli tunahitaji nguvu kubwa ya pamoja kuendesha harakati kuhakikisha Sheria ya Ndoa Mwaka 1971, inafanyiwa marekebisho kuondoa Kifungu Namba 14, kinachoruhusu msichana mwenye umri miaka 14 kuolewa kwa ridhaa ya wazazi wake", anasema Rebecca Gyumi, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Msichana Initiative.

Vilevile, Mtandao wa Wanawake, Katiba, Uchaguzi na Uongozi, ulitoa mchango mkubwa wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, kwa kuchangia kukishawishi chama tawala, kuona umuhimu wa kumteua mwanamke kugombea nafasi ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ambaye sasa ni Rais.

La tatu wanalojivunia, katika mafanikio ni WFT-T ilipokutanisha watu 300 kuanzia tarehe 24 hadi 26, mwezi uliopita, wakapanga mikakati ya kuiwezesha Tanzania kufikia usawa kati ya wanawake na wanaume kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Mtazamo huo unalenga kabla ya miaka 50 kuanzia sasa, ikiangazia kukoma vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake, wasichana na watoto vitakuwa imetokomezwa.

Anaitaja mikakati hiyo, inajumuisha mashirika yanayotetea haki za wanawake, wasichana na watoto kupata nguvu za pamoja kutafuta fedha za kutekeleza mipango yao, jambo muhimu kwa kila mdau wa maendeleo, ikiwamo serikali na wafadhali.

Pia, hapo kunatajwa shughuli za maendeleo na vyombo vya habari, vinavyounga mkono juhudi za WFT-T, zikilenga kuleta maendeleo ya kweli nchini, kwa kuzingatia usawa kati ya wanawake na wanaume kiuchumi, kisiasa na kijamii.

***• Ananilea Nkya, kitaaluma ni mwanahabari mzoefu, msomi wa ngazi ya Shahada ya Uzamivu (PhD), akizamia stadi, 'Namna Taarifa za Habari Zinavyochangia Maendeleo Tanzania.'***



Mwenyekiti wa WFT-T, Prof. Ruth Meena. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

DK. GRACE MZENGI

# Daktari aliyepata saratani ya matiti, asimulia siku alivyopokea vipimo

• Inatisha, anaifahamu, athari na hatima yake

**Na Mwandishi Wetu**

SARATANI ni tatizo linaloumiza maelfu ya wanawake duniani. Inashambulia matiti, shingo ya kizazi na viungo vingine mwilini. Kama sehemu ya Siku ya Wanawake Duniani, Nipashe inaelezea uzoefu wa wataalamu wa afya ambao wamepata tatizo hilo.

Nini hutokea madaktari wabobezi wanapokuwa wagonjwa wa saratani ya matiti? Jibu linatoka kwa Dk. Grace Mzengi na Profesa Julie Makani, katika mahojiano waliyofanya na Mtandao wa Medicopress.

Makala inaanza na Dk. Grace, anayeeleza kuwa ilikuwa Novemba 2007, wakati akiwa na miaka 43, alihisi uvimbe usio na maumivu tena mlaini kwenye titi la kushoto. Aliuguza na kuuchunguza kwa mkono jambo ambalo alikuwa analifanya tangu akiwa mwanafunzi wa shule ya udaktari miaka ya 1990.

"Sikuwa makini sana, ingawa nilidhani ni mabadiliko ya homoni na huenda ikawa uvimbe tu," anasema Dk. Grace akijibu swali kwanini hakuchukua juhudi za haraka kushughulikia titi mapema. Anasema katika hatua hiyo, kila kitu kilikuwa sawa, lakini aliendelea kufuatilia uvimbe kuangalia mabadiliko, ukubwa na mitoki chini ya kwapa. Hakukuwa na tatizo akafikiria siyo saratani, mwaka 2008 hakuchukua hatua .



Dk. Grace Mzengi. **PICHA: NA MPIGAPICHA WETU**

### HOSPITALI OCEAN ROAD

Anasema 2009 anafika katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road jijini Dar es Salaam, alifanyiwa upasuaji unaojulikana kama Fine Needle Aspiration (FNA) kuchukua sehemu ya uvimbe kwa uchunguzi.

" Matokeo yalionyesha kuwa hakuwa na saratani, badala yake kuna uvimbe usio kansa unaojulikana kama 'fibroadenoma'. Nilifurahi sana," anasema.

### UKWELI UNAOSIKITISHA

Kituo cha kazi cha Dk. Grace kilikuwa Chuo cha Afya Mafinga wilayani Mufindi, alikuwa mkuu wa taasisi na Septemba 2010, kulikuwa na timu ya madaktari wageni kutoka Ubelgiji ambao walikuwa wakifanya upasuaji kwa kushirikiana na madaktari wa ndani wilayani Mufindi.

"Inapendekezwa kitaalamu kuondoa uvimbe wa matiti kwa wanawake zaidi ya miaka 40, niliamua kuuondoa kwa kutumia mabingwa wa upasuaji," anasema, akielezea jinsi alivyoendelea kuuguza jeraha lake la upasuaji huku akidumisha usiri wake.

"Katika kipindi hicho nilikuwa na faragha kwa sababu wanafunzi wangu walikuwa likizo. Lakini katika hatua hii, matokeo ya yale ambayo daktari wa upasuaji alipata baada ya kuondoa tishu za matiti yake yalikuwa bado kunifikia."

Mnamo Oktoba 2010, daktari wa upasuaji aliyemfanyia Dk.Grace operesheni alitoa ripoti ya ugonjwa, akimtumia email na yalionyesha saratani katika hatua ya pili (2), inayojulikana kama 'adenocarcinoma' inayosambaa sehemu nyingine za mwili.

> Inapendekezwa kitaalamu kuondoa uvimbe wa matiti kwa wanawake zaidi ya miaka 40, niliamua kuuondoa kwa kutumia mabingwa wa upasuaji.

### KUUKUBALI UKWELI

"Ilikuwa baada ya saa za kazi, nilikuwa peke yangu ofisini niliposoma ripoti kutoka kwenye email. Haikuwa rahisi, nilihisi kizunguzungu na kulia. Ilikuwa kana kwamba niliambiwa kwamba "maisha yako yamebakiza miaka michache tu."

"Kukaa na taarifa hizi kulinitia wasiwasi zaidi. Niliamua kumshirikisha rafiki yangu wa karibu ambaye ni daktari anayefanya kazi Dar es Salaam. Nilimpigia simu nikamjulisha. Nilishangaa jinsi alivyokuwa mtulivu, na akaniambia nisiwe na wasiwasi ikiwa matibabu yataanzishwa mapema nitapona," anasema Dk. Grace.

"Siku iliyofuata, nilimweleza msaidizi wangu kazini habari hizo, akaisoma ripoti hiyo na kuniambia, "katika hatua hii ukipata matibabu utakuwa poa." Kusikia kutoka kwa madaktari wenzangu maneno hayo, nilianza kuona nuru mbele na tumaini jipya."

"Kwa kifupi, kuwa mtaalamu wa matibabu ambaye anaelewa michakato ya ugonjwa, hakuna tofauti katika hisia juu ya utambuzi. Nilijifunza kutoka kwa wengine ambao walisimulia hadithi zao za saratani, wengi wetu mwanzoni, tumekutana na kuguswa na uchungu kama vile kuelezea hofu na kulia."

### KILICHOFUATA?

"Baada ya kugunduliwa, sikuamua ni lini nianze matibabu. Niliendelea kuchelewa, Aprili 2011, nilienda katika Hospitali ya Apollo India. Madaktari walifanya uchunguzi zaidi kabla sijaanza tiba. Huu ulikuwa wakati mwingine mgumu," anasema Dk. Grace.

"Nilikuwa na wasiwasi wa matokeo ya uchunguzi wa daktari na nini kingetokea hasa kiwango cha ugonjwa huo na athari za tiba ya saratani ya 'chemotherapy'"

Lakini mwezi huo huo Dk. Mzengi alianza matibabu ambayo alimaliza Agosti 2011, akisema haikuwa rahisi kuvumilia. Kuna wakati alipata maambukizo na seli nyeupe za damu zilipopungua , lakini alifanya mazoezi na aliendelea kuhimili.

Dokta Grace alipitia matibabu ya upasuaji mwaka 2010, ikifuatiwa na tiba ya saratani 'chemotherapy' mwaka 2011, kisha tiba ya homoni na radiotherapy.

Kufuatia matibabu hayo, anasema, niliishi kwa miaka 10 bila matatizo ya kiafya. Kwa muda huo nilikuwa najipima matiti kila mwezi, sikuwahi kuhisi mabadiliko yoyote."

### SARATANI KUJIRUDIA

Mnamo Mei 2021, Grace alifanyiwa uchunguzi wa kila mwaka wa matibabu ya uchunguzi wa 'mammogram' au altrasound ya matiti na X-ray ya kifua ulifanyika. Matokeo yalikuwa ya kawaida.

Lakini Desemba 2021, wakati wa uchunguzi wa kawaida wa matiti wa kila mwezi, alihisi kuna uvimbe laini usio na maumivu chini ya kovu la awali la titi lile lililokuwa na tatizo.

Mnamo Februari 2022, uvimbe uliondolewa na kuchunguzwa katika idara ya saratani ya Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma, ripoti ya ugonjwa ikafichua kwamba saratani hiyo imejirudia."

"Nilipoteza matumaini kabisa. Usiku huo sikulala usingizi. Niliumia moyoni. Huu ulikuwa wakati mgumu zaidi maishani mwangu. Nilikuwa nikipima kuanza au kutoanza matibabu. Mwishowe, nilianza mzunguko wa kwanza wa chemotherapy. Bado sikufurahishwa na matibabu."

Dokta Grace anaongeza: "Baada ya mzunguko wa kwanza wa chemotherapy, nilikwenda Hospitali ya Agha Khan Dar es Salaam kutafuta maoni zaidi ya kitaalamu. Nilitaka kuondoa shaka kuhusu utambuzi na kuepuka chemotherapy. Shukrani kwa mtaalamu wa saratani 'oncologist' na upasuaji ambaye alinishauri. Nilipata tena nguvu za kufanyiwa matibabu hayo."

Anazidi kueleza: "Nilikuwa na mizunguko sita ya chemotherapy na 'mastectomy' kuondoa titi. Baada ya kukamilika kwa matibabu ya kemikali, miezi miwili baadaye nilipata ugonjwa wa moyo. Hili lilikuwa pigo lingine maishani mwangu kwani lazima nihudhurie kliniki za moyo na kutumia dawa kila siku."

Mtaalamu huyo wa afya anasema, amejifunza kuwa mtu yeyote anaweza kupata saratani ya matiti bila kujali hali yake. Saratani yoyote ni kama vita, ukipata matokeo ya uchunguzi, wakati wa matibabu, baada ya matibabu na hali yote maishani. Mtu anatakiwa kupambana nayo kwa ukali na kulenga kuishinda.

"Uchunguzi wa matiti unapaswa kuhamasishwa ili kugunduliwa mapema. Mfano mzuri ni pale nilipoona uvimbe huo miezi saba baada ya uchunguzi wa kimatibabu hospitalini."

Anataja somo jingine kuwa huwezi kupigana peke yako, unahitaji watu, wahudumu wa afya, wanafamilia, marafiki, viongozi wa kiroho na jamii inayokuzunguka. Wote wana jukumu la kufanya kufanikisha mchakato wako wa matibabu.

"Kuwaeleza wengine habari hasa ndugu, marafiki, wafanyakazi wenzako na viongozi wa kidini ni muhimu kupunguza unyanyapaa na huzuni.Watu wanapaswa kutafuta habari kutoka kwa vyanzo vya kuaminika. Kuna hadithi na habari potofu katika jamii zetu kuhusu ugonjwa na matibabu." Anasema Dk. Grace.

### KUHIMILI MABADILIKO

Anasema: "Kabla ya matibabu nilikuwa na afya njema na mwenye bidii. Baada ya matibabu, nilikuwa na mabadiliko mengi kama upara, rangi ya ngozi na kucha, kujisikia joto kali bila kujali hali ya hewa ya baridi huko Mafinga. Kwa watu walionifahamu, wangeweza kuuliza kilichotokea. Mbali na jamii, nilikuwa nikifundisha wanafunzi wa udaktari. Lazima nihudhurie vipindi vyangu licha ya sura na hisia zangu kubadilika."

"Haikuwa ngumu kufichua nilichokuwa nikipitia kwa sababu nilitaka wanafunzi wangu wajifunze kuhusu saratani ya matiti kutoka upande wa wataalamu, kinga, uchunguzi, utambuzi na usimamizi. Pia ninahimizi kujichunguza matiti ili kutambua tatizo mapema. Pia nilitumia kurasa zangu za mitandao ya kijamii kufichua na kuongeza ufahamu kila Oktoba," anasema Dk. Grace.

# RC awapa jukumu wanawake kutokomeza vitendo vya ukatili

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyemule, amewataka wanawake kuhakikisha wanashirikiana na serikali na vyombo vya dola kutoa taarifa dhidi ya vitendo vya ukatili.

Aidha, amewataka wanawake kumuomba Mungu kwa uaminifu ili tatizo la vitendo hivyo na matendo mengine ya kiahalifu yaweze kutoweke na watu waiishi kwa amani, utulifu upendo na mshikamano.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wanawake kutoka madhehebu mbalimbali ya dini kwenye maadhimisho ya wiki ya maombi duniani yaliyofanyika kwenye Kanisa la Kiinjili Kilutheli Tanzania (KKKT) mkoani Dodoma.



Alisema vitendo vya kikatili vinavyotokea waathirika wakubwa ni wanawake, watoto na watu wenye ulemavu.

"Hivi niwaombe wanawake wenzangu tushirikiane na Rais Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha vitendo hivyo wanavyofanyika vya kikatili vinatolewa taarifa hata kama wanaofanya ni watoto wetu au ndugu zetu. Tunataka nchi hii Watanzania waendelee kuiamini serikali yao pamoja na amani iliyopo," alisema.

Pia aliwataka wanawake kuhakikisha wanagombea nafasi mbalimbali za uongozi badala ya kuziachia kwa wanaume.

Alisema ni wakati sasa kwa wanawake kuachana na dhana kuwa wao hawawezi kuongoza nafasi yoyote, hivyo aliwataka wajitokeze kwa wingi ili waweze kuchangamkia fursa.

Pia aliwaomba wanawake wa Mkoa wa Dodoma kutumia fursa za uwekezaji katika kujiongezea kipato kupitia miradi mikubwa iliyopo ikiwamo ya ujenzi wa reli ya kisasa, mabwawa ya umwangiliaji na miundombinu ya barabara za mizunguko.

Mchungaji kutoka Kanisa la Anglican, Agness Liheli, akihubiri katika kongamano hilo alisema kuwa vitendo vya kikatili vinavyojitokeza chanzo kikubwa ni ukosefu wa maadili.



Ofisa Tarafa wa Wilaya ya Dodoma, Zainabu Issa (wa tatu kulia), akikagua jiwe la mpaka wa kiwanja cha kanisa la Pentecost Christian International (PCI), eneo la Mji Mwema, Mtaa wa Mtakuja Changombe ikiwa ni sehemu ya kutatua migogoro ya mipaka kwenye mtaa huo jana. Wengine ni baadhi ya watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Dk. Gwajima ataja vikwazo vinavyowasibu wanawake

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema gharama kubwa ya kutojua kusoma na kuandika, ukosefu wa ujuzi pamoja na ukosefu wa faragha na usalama ni mojawapo ya vikwazo kwa wanawake kufikia teknolojia za dijitali.

Alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani leo.

Alisema baadhi ya wanawake na wasichana bado hawanufaiki na teknolojia ya kidijitali jambo linalowafanya kuzikosa baadhi ya fursa za kiuchumi na ajira.

Kadhalika alisema ulimwengu wa leo katika karne uko kwenye zama za teknolojia ya kidijitali ambayo inachochea kwa kasi mabadiliko ya kijamii na kiuchumi, hivyo ni muhimu kuhakikisha kuna usawa wa kijinsia kwenye maendeleo ya teknolojia ya kidijitali.

Alisema katika nchi zenye uchumi wa chini ya asilimia 76 watu wake wana simu zinazopokea mtandao lakini asilimia 25 tu ndiyo wanatumia mtandao, huku asilimia 52 wakiwa ni wanaume hivyo wanawake ni wachache zaidi.

Alisema sababu zingine zinazosababisha wanawake kuwa nyuma kwenye matumizi ya kidijitali ni kutoona umuhimu wa kumiliki simu, kutofahamu upatikanaji wa nishati ya umeme, mila, desturi na vikwazo vingine.

Pia alisema mwaka 2022 takwimu zinaonyesha asilimia 63 ya wanawake duniani walitumia mtandao ukilinganisha na asilimia 69 ya wanaume, huku uwezo wa wanawake kumiliki simu ukiwa chini kwa asilimia 12 ukilinganisha na wanaume.

Aliongeza kuwa pengo la wanawake kumiliki simu na kutumia mtandao linaonekana zaidi kwa wanawake wenye umri mkubwa (wazee), wanawake wanaoishi vijijini pamoja na wanawake wenye ulemavu.

Dk. Dorothy alisema vikwazo vya wanawake kwenye kutumia mtandao vinawaathiri kwenye fursa za maendeleo na kupata huduma mfano; idadi ya nchi zinazotoa walau huduma moja ya kijamii kwa njia ya mtandao zimeongezeka kutoka 162 mwaka 2020 hadi 189 mwaka 2022.

Aliongeza kuwa watumiaji wa huduma za mtandao hasa wanaume wana faida kubwa kupata taarifa za afya, elimu, kilimo, biashara, ajira na zingine hivyo kuna kila sababu ya kuhakikisha wanawake wanawezeshwa kidigitali ili kufikia usawa wa kijinsia kwenye maendeleo.

Alisema wanawake wajasiriamali 21,546 kutoka mikoa 26 ya Tanzania Bara wamepata mikopo yenye masharti nafuu yenye thamani ya Sh.milioni 78. 6 kati ya mwaka 2018/19 - hadi 30 Aprili 2022.

Alisema mikopo yenye jumla ya Sh. milioni 663.4 imetolewa kwa vikundi vya wanawake wajasiriamali 11 na mjasiriamali mmoja kuanzia Julai mwaka jana hadi Januari mwaka huu.

Hata hivyo, alisema huduma za kifedha kidijitali nchini zimeimarika kuwafikia wanawake mijini na vijijini na takwimu zinaonesha asilimia 99 ya watu wazima wanafahamu kuhusu huduma ya kifedha kupitia simu za mkononi na asilimia 45 kati yao wanazitumia kikamilifu.

# Watanzania wapewa hadhari magonjwa yasiyoambukiza

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kuchukua tahadhari ya kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza ili kuiondolea mzigo serikali wa kutumia fedha nyingi kuhudumia wagonjwa.

Mwenyekiti wa mtandao wa magonjwa yasiyoambukiza, Prof. Andrew Swai, aliyasema hayo juzi wakati akiwasilisha mada kwenye kongamano la siku moja jijini hapa lenye lengo la kujadili athari na gharama za magonjwa yasiyoambukiza.

Alisema serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kutibu magonjwa hayo, hivyo wananchi wanapaswa kuchukua hatua ili kujikinga nayo.

Alisema gharama hizo pia zimekuwa zikitumiwa na wananchi na familia za wagonjwa wa magonjwa hayo.

Prof. Swai alisema gharama hizo zikiepukwa zitasaidia uchumi wa nchi na jamii na maisha kuboreshwa.

Alibainisha kuwa asilimia 34 ya wagonjwa kwenye hospitali nyingi nchini inatokana na watu kuugua magonjwa hayo.

Aliyataja baadhi ya magonjwa hayo kuwa ni kisukari na shirikizo la damu ambayo yamekuwa sugu na wakati mwingine yamekuwa yakiwasababishia watu upofu.

Kadhalika, alizitaja mbinu za kuepuka kupata magonjwa hayo kuwa ni kuzingatia kula vyakula visivyo na mafuta mengi.

Pia alitaja mbinu ya kufanya mazoezi na kula matunda kwa wingi kuwa inasaidia kulinda mwili na magonjwa hayo.

Mkurugenzi wa magonjwa yasiyoambukiza, Prof. Paschal Rugajo, alisema kwa sababu ya uzembe wa wananchi kupuuzia ushauri huo wa kitaalamu umechangia kwa kasi magonjwa hayo.

Prof. Rugajo alisema serikali imekuwa ikitoa mafunzo hayo kwa ajili ya kukinga afya za wananchi dhidi ya magonjwa hayo. Hivyo, aliwaomba mama lishe walioshiriki kongamano hilo kutumia elimu waliyopata kwa ajili ya kunusuru maisha ya wateja wao.

Alisema watu wengi wamekuwa wakipata huduma za chakula maeneo mbalimbali, hivyo wapishi hao wananafasi ya kusaidia kulinda afya za watu.

Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Jamal Ngalya, alisema kuna baadhi ya watu wanakunywa pombe kupita kiasi kitendo ambacho ni hatari kwa afya zao.

Aidha, aliwashukuru wataalamu hao kwa kutoa elimu ambayo itasaidia kuokoa afya za watu na gharama za matibabu zinazotolewa na serikali pamoja na wananchi hao wakati wa ugonjwa.





# Madereva bodaboda watakiwa kukemea kauli chonganishi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MWENYEKITI wa madereva pikipiki 'bodaboda' Mkoa wa Mbeya, Aliko Fwanda, amesema vijana wa bodaboda wanapaswa kukemea kauli za baadhi ya viongozi wa kisiasa wenye uchu wa madaraka wanaodai kuwa kazi hiyo ni ya laana.

Hivyo amewataka kutoa ushirikiano kwa serikali na viongozi waliopo madarakani.

Alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na Nipashe baada ya kuibuka kauli kwamba kazi ya bodaboda ni ya laana.

"Jimbo la Mbeya Mjini hatuwezi kuwa wanafiki na tukiwa wanafiki tutaadhibiwa na Mungu, tunahitaji viongozi mfano wa Dk. Tulia Ackson ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutupatia mitaji ya kuendesha biashara," alisema Fwanda na kuongeza:

"Mimi ni mwanachama wa CHADEMA na wengi mnanifahamu lakini nitaongea ukweli kwamba muda wa mihemko umeisha, tulikuwa tunachagua viongozi kwa mihemko imetugharimu lakini sasa hivi Mbeya tunajitambua na tulikuchagua Dk. Tulia wewe na utaendelea kuwa mbunge wetu,"alisema Fwanda.

Aliongeza kuwa yeye ni kiongozi wa bodaboda na amepata manufaa mengi kupitia Taasisi ya Tulia Trust ikiwamo kupewa mikopo ambayo hadi sasa imemwezesha kumiliki bajaji 120 na bodaboda zaidi ya 200.

"Anapotokea mtu anasema bodaboda ni ajira ya laana yeye ndiyo mwenye laana kwasababu hatuwezi wote sisi kuwa wabunge, tumejiajiri kutokana na watu wanaotuwezesha na tunapaswa kumshuruku Mungu hatuhitaji chokochoko bali tunahitaji kuwa na viongozi makini," alisema Fwanda.

Hivi karibuni Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini ambaye ni Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson aliwawezesha wanawake wajasiriamali 1,000 kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya.

Kila mwanamke alipatiwa Sh.100,000 kwa ajili ya kukuza biashara yake ambapo kiasi cha Sh.milioni 100 kilitengwa kwa ajili ya kuwasaidia.

Aliwataka wanawake hao kutumia fedha hizo kwa malengo yalikusudiwa na kuwaahidi kuwa endapo watafanya vizuri ataendelea kuwaongezea mitaji na kuwafikia wengi zaidi ili wajikwamue na umaskini.



Mwakilishi wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, ACP Christina Msyani (kulia), akishirikiana na askari wanawake kutoa misaada mbalimbali zikiwamo taulo za kike, sabuni na mafuta ya kupakaa kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wilayani Chunya juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Mbaroni tuhuma kukutwa na dawa za kulevya kilo 15

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya linamshikilia mkazi wa Sambilimwaya wilayani Chunya, Mkoa wa Mbeya, Filimoni Lambasika (38) kwa tuhuma za kupatikana na dawa za kulevya aina ya bangi yenye uzito wa kilogramu 15.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Benjamin Kuzaga, aliyasema hayo jana na kwamba mtuhumiwa alikamatwa Machi 02, 2023, saa saba mchana baada ya msako uliofanyika katika Kitongoji cha Sambilimwaya, Kijiji cha Chokaa, Wilaya ya Chunya.

"Mtuhumiwa alikamatwa akiwa anafanya biashara ya kuuza dawa hizo za kulevya akiwa ameifunga kwenye mifuko ya nailoni alimaarufu rambo na mfuko wa sandarusi, tayari tumemkamata na tunasubiri taratibu za upelelezi kukamilika ili kufikishwa mahakamani," alisema.

Aliongeza kuwa Jeshi la Polisi pia linamshikilia Hewad Jackson (33), mkazi wa Kijiji cha Ilembo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa tuhuma za kupatikana na ng'ombe 10 wa wizi wenye thamani ya shilingi milioni 15.

Alisema awali katika Kijiji cha Ntokela wilayani Rungwe, askari walimtilia shaka mtuhumiwa baada ya kumuona akiwaswaga ng'ombe 10 na ndipo kumkamata.

Aliongeza kuwa alijitokeza aliyeibiwa ng'ombe hao aitwaye Thadeo William (50) Mkazi wa Kijiji cha Shango ambaye alizitambua ng'ombe hizo kuwa zimeibiwa katika Kijiji cha Kikondo kilichopo Kata ya Ilungu.

"Mtuhumiwa anaendelea kuhojiwa ili kujua watu anaoshirikiana nao katika matukio ya wizi wa mifugo pamoja na kujua maeneo anayouza ng'ombe hao," alisema Kamanda Kuzaga.

# Vijana wapewa siri kujikwamua kiuchumi, kuwa matajiri

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

VIJANA mkoani Mbeya wameshauriwa kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza kupitia mashirika na taasisi ili kujikwamua kiuchumi badala ya kujiingiza kwenye makundi yasiofaa na kuharibu ndoto za maisha yao.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkurugenzi wa Kampuni ya Rafael Group, inayojihusisha na uuzaji na usambazaji wa nafaka jijini Mbeya, Rafael Ndelwa.

Alisema ili vijana waweze kutimiza malengo yao lazima kuheshimu ndoto za maisha yao badala ya kushawishika na wenzao na kujiingiza kwenye makundi yasiyofaa.

"Mimi ni miongoni mwa vijana wa mfano mkoani Mbeya, nilianza kufanya shughuli ndogo kabisa za uuzaji wa usambazaji wa nafaka nilikuwa na mtaji mdogo lakini kwa kuwa nilikuwa na maono ya kufika mbali nilihakikisha natimiza azma yangu ambayo imenisaidia sasa namiliki kampuni kubwa ambayo pia imeajiri vijana wengi," alisema Ndelwa.

Alisema kwa sasa kampuni yake ina uwezo wa kukopesha pembejeo za kilimo wakulima wa mazao kama vile maharage, mpunga, ngano ambapo baada ya mavuno wakulima hao humpatia mavuno kulingana na gharama za pembejeo zilizotolewa.

Alisema zaidi ya wakulima 100 wamenufaika na fursa hiyo na kumwezesha yeye kuwa na akiba ya mazao mengi ambayo huyachakata kisha kuuza ndani na nje ya nchi.

Sambamba na hilo pia alisema ameweza kuweka mashine kubwa za kisasa kwa ajili ya kusaga nafaka kama vile mpunga katika kampuni yake na kuyapaki kwenye vifungashio.

Aliwashauri vijana kuchangamkia fedha za asilimia 10 za mikopo inayotolewa na halmashauri kwa kuhakikisha wanajiunga kwenye vikundi ili waweze kukopesheka na kuanzisha shughuli za kujikwamua na umaskini.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo, alisema katika kuhakikisha wananchi wa mkoa huo wanafanya shughuli zao wakiwa na afya alitoa Sh. milioni 15 kwa ajili ya kuwakatia bima wananchi 500.

## ZBS kukamilisha ufungaji vifaa maabara chakula

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAASISI ya Viwango Zanzibar (ZBS) imesema ipo katika hatua za mwisho za ufungaji wa vifaa katika maabara ya kupima vyakula vinavyozalishwa au kuingia nchini, ili kudhibiti bidhaa zisizo na ubora.

Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Yussuph Majid Nassor, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanyika kwa mkutano wa jukwaa la viwango.

Alisema kukamilika kwa maabara hiyo kutaiongezea uwezo taasisi hiyo kufanya kazi ya ukaguzi wa bidhaa badala ya kutumia mawakala waliopo nje ya nchi au kupeleke sampuli kwenye maabara nyingine.

Alieleza kuwa hatua hiyo inatokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali kwa taasisi hiyo kwa lengo la kuhakikisha usalama wa watumiaji wa bidhaa ikiwamo za vyakula.

Aidha, alifahamisha kuwa mbali ya maabara hiyo inayotarajiwa kuanza kazi Aprili mwaka huu, taasisi hiyo inatarajia kujenga kituo cha kisasa cha ukaguzi wa magari na mitambo.

Alisema ili kuzitumia maabara hizo kwa ufanisi, taasisi inaendelea kuajiri na kuwapatia mafunzo watendaji wake ndani na nje ya nchi ili kuwa na utaalamu wa kutosha utakaowapa uwezo wa kufanya kazi zao kwa ufanisi.

"ZBS imejipanga kuhakikisha inatoa huduma kidijitali ili kurahisisha utoaji wa huduma na kuondoa usumbufu kwa wateja," alisema.

Akizungumzia kutambulika kwa cheti cha bidhaa zinazokaguliwa na ZBS, alisema cheti kinachotolewa kinatambulika kitaifa na kikanda na kwamba wapo katika hatua za mwisho kupata cheti cha ithibati ya kimataifa kutoka kwa Shirika la Viwango Kimataifa (ISO).

Alifafanua kuwa hatua hiyo itaziwezesha bidhaa za Zanzibar zitakazopata alama ya ubora kutambulika kimataifa, hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa biashara nchini na kuipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kuendelea kuiimarisha taasisi hiyo.

Ofisa Uhusiano wa ZBS, Umulkulthum Hamza Mohamed, alisema taasisi hiyo iliaanzishwa ili kuhakikisha kunakua na bidhaa bora na zinazokidhi viwango na mahitaji ya wananchi.

Alieleza kuwa toka kuasisiwa kwa taasisi hiyo mwaka 2012 na kuanza kazi mwaka 2013, jumla ya viwango 497 vimeidhinishwa na kuanza kutumika.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC), Abdallah Abdulrahman Mfaume, aliiomba ZBS kuendeleana kushirikiana na vyombo vya habari kujitingaza ili jamii ielewe kazi inazofanya.

# 'Unguja, Pemba ni vivutio vikubwa vya utalii duniani'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Mhandisi Shomar Omar Sharif, amesema visiwa vya Unguja na Pemba ni miongoni mwa vivutio vikubwa vya utalii duniani.

Amesema visiwa hivyo ni kitovu kikubwa cha biashara ya utalii katika Ukanda wa Bahari ya Hindi, hivyo ni vyema kuthamini mchango mkubwa wa usafiri wa anga na utalii katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii Zanzibar.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya utoaji huduma bora kwa watoa huduma wa Uwanja vya Ndege wa Abeid Amani Karume ambayo yaliandaliwa na mamlaka ya viwanja hivyo kwa kushirikiana na Kampuni ya DNATA kutoka Dubai ambayo inatoa huduma katika uwanja hivyo.

Alisema sekta ya utalii inaathari kubwa katika sekta zingine za kimaendeleo iwe rasilimali, mazingira na utamaduni, hivyo uhusiano mwema na mwenye mazingira wezeshi ni muhimu katika uendeleza sekta zingine za maendeleo.

Hivyo aliwataka wadau wa uwanja huo wakiwamo Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Polisi, mashirika ya ndege, madereva taksi, watembeza watalii kuwa mfano wa kuigwa katika utoaji wa huduma wenye hadhi na kiwango cha kimataifa.

Alisema serikali inamipango thabiti na imara katika kuimarisha viwanja vya ndege vya Zanzibar.

Philemon Azer kutoka Kampuni ya DNATA alisema wamejipanga kutoa huduma bora ikiwamo za wageni na watalii wanaoingia nchini na wameimarisha huduma kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji ili kuepuka kukaa muda mrefu kusubiri huduma.

Alisema kwa sasa wanahudumia mashirika ya ndege 12 katika Uwanja wa Ndege wa Abeib Amani Karume Zanzibar.

"Tumeamua kutoa mafunzo haya kwa watoa huduma wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ili kwenda na kasi ya utoaji huduma bora katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar,"alisema.

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Nasra Muhammed Hassan, alisema mafunzo hayo yataongeza utendaji katika kutekeleza majukumu na wajibu kwa wafanyakazi wa viwanja hivyo.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), Arafat Haji (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Zanzibar juzi, wakati wa utambulisho wa huduma yao mpya ya bima ya magari mahususi kwa wanawake ijulikanayo kama "Queen Motor Insurance" pamoja na uwasilishaji wa taarifa ya mafanikio kwa mwaka 2022. Wengine ni Mkurugenzi Idara ya Biashara na Uwekezaji, Mohammed Ameir (wa pili kulia), Meneja wa TEHAMA, Bakar Yussuf (kulia), Mkurugenzi wa Rasilimali Watu, Salma Mwinyi (wa pili kushoto) na Katibu wa Shirika hilo, Asha Rashid. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# ZIC yazindua bima mpya mahususi kwa wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

KUELEKEA maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) limezindua huduma mpya ya bima ya magari mahususi kwa wanawake.

Bima hiyo iitwayo 'Queen motor insurance' huku likijivunia mafanikio makubwa liliyopata katika kipindi cha mwaka mmoja ikiwamo ongezeko la asilimia 169 kwenye mapato yatokanayo na ada za bima.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bima Zanzibar (ZIC), Arafat Haji, akizungumza wakati wa uzinduzi huo alisema ujio wa Queen motor insurance unalenga kutoa ulinzi na kinga kwa magari binafsi yanayomilikiwa na wanawake endapo yatakabiliwa na majanga mbalimbali ikiwamo moto, ajali na wizi.

"Zaidi pia tutahusika na hasara itakayosababishwa na mteja kwa watumiaji wa barabara, pamoja na mali zao kwa kuwa hii ni bima kubwa," alibainisha.

Kwa mujibu wa Arafat uzinduzi wa huduma hiyo umekuja wakati ikiwa ni ishara ya shirika hilo kuungana na dunia kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Akizungumzia mafanikio ya shirika hilo kwa mwaka 2022, Arafat alisema shirika limekusanya mapato yatokanayo na ada za bima Sh. bilioni 40.2 sawa na ukuaji wa asilimia 169.55 ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa mwaka uliopita ambapo shirika hilo lilikusanya Sh. bilioni 23.7.

Alisema mafanikio hayo yameambatana na ukuaji wa uwekezaji wa shirika hilo ambapo kwa mwaka 2022 shirika hilo liliweza kukuza uwekezaji wake kwa asilimia 64.51 ikilinganishwa na mwaka uliopita.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**JEROME BARNABAS GABRIEL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index number **S0413-0748** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KIBITI SEKONDARI mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KAG/KAI/RB/526679/2020.**

## PATA MKOPO KWA HARAKA

PATA MKOPO KWA HARAKA
**HADI 200,000,000/=**
KUTOKA
**ENTERPRISE FINANCE LIMITED**
KWAAJILI YA DHARURA MBALIMBALI KAMA KULIPA KODI YA NYUMBA, KUNUNUA GARI, KUBORESHA BIASHARA N.K

117303202

**TUNAPATIKANA**
DAR ES SALAAM **0677111333**
NA ARUSHA **0677226960.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YUSTINA ADAM TIZEBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T.623 BYV** aina ya Honda **CRV Rangi nyeusi.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Yustina Tizeba kwa simu namba **0753-829014.**
Taarifa ya polisi
**SHI/SHI/RB/81651/2023**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.19 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late GRATIAN GABRIEL RWEYEMAMU of Dodoma City**

**AND**

**In the matter of an application for letters of administration by GRACE GRATIAN RWEYEMAMU.**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 11TH Day of APRIL, 2023

Dated at Dodoma this 07TH day of MARCH, 2023

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**

**SHAURI NO;10/2023**

**JACOB J. MWAISANGO.............................................MDAI**

**DHIDI YA**

**ELIAH MASTER MAHOZI........................................MDAIWA**

**YAH;KUITWA SHAURINI**

**KWA; ELIAH MASTER MAHOZI,**

Fahamu kwamba JACOB J. MWAISANGO amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 14/03/2023 saa 2;30 asubuhi mbele ya T.Munzerere Mwenyekiti wa baraza. Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi ya baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba mbeya mjini.
Kumbuka;Usipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 06/03/2023.

T. Munzerere
MWENYEKITI
06/03/2023
CHAIRMAN
DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL
TANZANIA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NTEMI EZEKIEL MASSANJA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MERCEDES BENZ** yenye namba za usajili **T 879 CQN**, CHASSIS NAMBA: **WDB2110652AA65749** na ENGINE NAMBA: **671323301572.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochopte cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**DAR/URA/RB/453620/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MOSHI MOHAMED SIFI** anatangaza kupotelewa na Kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 602 CYR** aina ya **TVS** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Moshi Sifi kwa simu namba **0625542029.**
Taarifa ya Polisi
**SHI/SHI/RB/86293/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SELF ALLY KHALFAN** anatangaza kupotolewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 851 BNK** aina ya **TRAILER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya polisi.
**NGR/RB/500/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**EDITH JACOB MWAISANGO** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji aina ya Sinoray yenye namba za usajili **MC. 807 CCM** Chassis No. **LZSHCMZW 3J8009169.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
**RB No.MOR/MOR/RB/88042/2023**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie*
***0745 700 710.***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0745 700 710.

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

HABARI KIMATAIFA

## Rais wa China Xi ailaani Marekani

**BEIJING,** CHINA

RAIS wa China Xi Jinping amelaani kile alichokitaja kuwa ukandamizaji dhidi ya nchi yake unaoongozwa na Marekani, huku akisisitiza sekta binafsi nchini humo kuongeza ubunifu na kujitegemea.

Rais Xi aliyasema hayo jana wakati wa mkutano mkuu wa chama cha kikomunisti, huku akiwaambia viongozi wa sekta ya viwanda ya China, kwamba nchi za Magharibi zikiongozwa na Marekani, zimeweka vikwazo vya pande zote ikiwa ni pamoja na kuizingira na kuikandamiza nchi yao.

Pia alisema suala hilo limesababisha changamoto kubwa zisizo za kawaida kwa maendeleo ya nchi hiyo, na kwamba kipindi cha miaka mitano iliyopita, kiligubikwa na vikwazo vipya ambavyo vinatishia kudhoofisha ukuaji wa uchumi wa China.

Aidha, Rais Xi alitoa hotuba kwa wajumbe wakati wa kongamano la ushauri wa kisiasa wa watu wa China (CPPCC), akisisitiza kuwa lazima China iwe na ujasiri wa kupigana wakati taifa hilo likikabiliwa na mabadiliko makubwa na magumu katika mazingira ya ndani na ya kimataifa.

"Pia kampuni za kibinafsi zinapaswa kuchukuwa hatua ya kuzingatia maendeleo ya kiwango cha juu," alisema.

Hata hivyo, kiongozi huyo alisema nchi hiyo inapaswa kuwa na uwezo wa kujisimamia yenyewe, na kwamba kila wakati amekuwa akisema kuna sehemu mbili muhimu kwa China ambazo ni kulinda raslimali zao na kujenga sekta ya viwanda yenye nguvu.

Inaelezwa kuwa katika miezi ya hivi karibuni, Marekani imeimarisha vikwazo dhidi ya China ikitaja masuala ya usalama wa kitaifa na athari ya teknolojia inayotumiwa na jeshi la China.

Wakati huo huo, waziri wa mambo ya nje wa China Qin Gang, alisema kuwa kile kinachoamua uhusiano kati ya China na Marekani kinapaswa kuwa maslahi ya pamoja, majukumu ya pamoja na urafiki kati ya mataifa hayo mawili badala ya siasa za ndani na shutuma za kiholela.

Qin ambaye pia ni balozi wa zamani wa China nchini Marekani, alipuuzilia mbali tahadhari kutoka kwa mataifa ya Magharibi kwamba China huenda ikaisaidia Russia na silaha kwa vita vyake nchini Ukraine, akieleza kuwa taifa lake halitakubali lawama, vikwazo, ukandamizaji na vitisho.

Mwezi uliopita, China ilielezea msimamo wake kuhusu vita nchini Ukraine, kwamba ni taifa lisiloegemea upande wowote huku ikizihimiza pande mbili katika vita hivyo kuingia katika mazungumzo ya amani. **DW**

# PDP waandamana kupinga matokeo Nigeria

**LAGOS,** NIGERIA

WANACHAMA wa chama cha upinzani cha People's Democratic Party (PDP) wameandamana hadi ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi nchini Nigeria (INEC) kupinga matokeo rasmi ya uchaguzi wa urais.

Tume hiyo ilimtangaza mgombea wa chama tawala cha All Progressives Congress (APC) Bola Tinubu, kuwa mshindi wa uchaguzi wa Februari 25, mwaka huu, ambao ulikumbwa na matatizo ya kiufundi yaliyochelewesha upigaji kura.

Vyama vya upinzani vilidai kuwa uchaguzi huo uliibiwa na kuibua changamoto za kisheria. Maandamano hayo yaliyoongozwa na mgombea urais Atiku Abubakar na maofisa wengine wa chama yaliandaliwa kupinga tangazo la wiki iliyopita la mgombea wa chama tawala Tinubu kama mshindi wa kura za urais.

Waandamanaji hao wengi wao wakiwa na mavazi meusi, waliimba kwamba Abubakar alishinda kura, na kwamba INEC ni mlaghai aliyepindua matakwa ya watu.

Msemaji wa kamati ya Kampeni ya urais ya PDP Kola Ologbondiyan, alisema wana ushahidi kwamba walishinda uchaguzi huo, huku wakiilaumu tume kwa kushindwa kutimiza wajibu wake.

"Tuna ushahidi kwamba tulishinda uchaguzi huu kwa kishindo, lakini tunachosema na tunachodai ni kwamba kwa sasa, Mahmood Yakubu hajafanya mapitio ya matatizo yaliyopo anapaswa kupitia tena makosa hayo, hayo ndiyo matakwa yetu," alisema Ologbondiyan.

Mshauri wa Abubakar, Paul Ibe, alisema "Huu ni uchaguzi mbaya zaidi katika historia yetu ya kidemokrasia. Kulikuwa na matarajio mengi. Wananchi wa Nigeria walikuwa wanatafuta kiongozi ambaye atawaleta pamoja na kuanza mchakato wa uponyaji. Kile tulichonacho kwa kweli ni wizi".

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Polisi waliokuwa na silaha waliwazuia waandamanaji hao kuvamia majengo ya INEC, na kwamba tume haikutoa ufafanuzi wowote juu ya malalamiko hayo.

Vile vile, ilibainishwa kuwa mwishoni mwa wiki iliyopita, INEC ilifanya kikao na viongozi kukagua uchaguzi huo na kujiandaa vyema kwa uchaguzi wa ugavana unaotarajiwa kufanyika Machi 11.

Pia inaelezwa kuwa wiki iliyopita, mgombea wa tatu Peter Obi alitangaza kuwa alishinda uchaguzi na atathibitisha hilo kwa Wanigeria mahakamani.

Balozi wa Marekani nchini Nigeria, Mary Leonard, alisema uchaguzi wa rais nchini humo umeshindwa kukidhi matarajio.

Rais mteule Tinubu alitoa wito wa kuwepo kwa umoja na kusema anataka pande zote kufanya kazi naye kwa ajili ya kuwa na nchi bora.

Wataalamu wanasema bila kujali jinsi mambo yatakavyokuwa, rais atakuwa na masuala makubwa ya kushughulikia, ikiwa ni pamoja na kuenea kwa ukosefu wa usalama, uchumi dhaifu, mifumo ya afya na elimu iliyo na matatizo. **VOA**




Wafuasi wa Chama cha Peoples Democratic Party (PDP) wakiandamana kuelekea makao makuu ya Tume Huru ya Uchaguzi (INEC) kupinga matokeo ya uchaguzi wa urais nchini Nigeria jana. **PICHA: REUTERS**

## Utapiamlo wakithiri mataifa maskini

**UNICEF**

SHIRIKA la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) limesema idadi ya wanawake wajawazito na wasichana wenye utapiamlo imeongezeka kwa asilimia 25 kwa miaka 20 iliyopita.

Katika taarifa ya shirika hilo iliyotolewa jana, ilisema idadi hiyo imeongezeka zaidi katika nchi masikini zikiwemo Somalia, Ethiopia na Afghanistan.

UNICEF inakadiria kuwa zaidi ya wanawake bilioni moja na vijana wenye umri wa kubalehe kote duniani wana utapiamlo.

Inasema mizozo ya hivi karibuni vikiwemo vita na janga la COVID-19 vimesababisha hali ya ukosefu wa chakula kinachohitajika kuwa mbaya zaidi.

Pia shirika hilo limetoa wito kwa jamii ya kimataifa kufanya usalama wa chakula kuwa kipaumbele cha kwanza, ikiwa ni pamoja na kusaidia mipango ya usaidizi wa chakula chenye virutubisho.

Aidha, UNICEF ilitoa angalizo pia kuhusu athari za utapiamlo kwa watoto.

Ripoti ya Unicef pia ilibaini kwamba wanawake bilioni moja wenye utapiamlo na wasichana walikuwa na uzani wa chini ya mwili na walikuwa na kimo kifupi kutokana na tatizo hilo, kulingana na uchanganuzi wa data za wanawake katika nchi nyingi duniani. **BBC**

# SIMBA QUEENS, JKT QUEENS MECHI YA KISASI, MBIO KILELENI

**Na Saada Akida**

HAKUNA neno litakalofaa kulitaja zaidi ya 'vita', pindi unapoelezea mchezo raundi ya pili wa Ligi Kuu Bara kwa upande wa wanawake, ambao utawakutanisha wenyeji, JKT Queens dhidi ya Simba Queens katika Uwanja wa Mej Isamhuyo, Dar es Salaam kesho.

Mchezo huo, utakuwa wa vita mbili kubwa, ambapo ni kisasi kwa upande wa Simba Queens ambao walifungwa mabao 2-1 kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza wakiwa katika uwanja wao wa nyumbani, Mo Simba Arena uliopo Bunju nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Vita ya pili, ni kusaka uongozi wa ligi ambapo kwa sasa timu hizo zinatofautiana alama moja, Simba wakiwa kileleni na pointi zao 22 wakati JKT wakiwa wanashika nafasi ya pili baada ya kujikusanyia alama 21, hivyo timu yoyote itakayoshinda itakaa kileleni.

JKT Queens wakati wa mapumziko ya ligi walikwenda visiwani Zanzibar kuweka kambi na wamerejea jana, Jumanne wakati Simba wao waliendelea kubaki Dar es Salaam wakijiandaa pia.

Mechi nyingine ambazo zitachezwa kesho, Jumatano ni Baobab Queens watakaokipiga dhidi ya Aman Queens kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, huku Ceasiaa wakicheza na Alliance Girls kwenye Dimba la Chuo cha Mkwawa Iringa.

Yanga Princess wao watakuwa na kibarua kinachofanana na Simba Queens, kwani watakuwa ugenini katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro dhidi yaFountain Gate Princess.

Hawa nao wana vita ya alama na kisasi, Yanga Princess walipoteza kwa bao 1-0 wakiwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, hivyo watahitaji kulipa.

Hata hivyo, kubwa ni alama tatu, wakati huu timu hizo zikiwa zinafanana alama baada ya kila moja kujikusanyia pointi 20, lakini Fountain Gates wakiwa nafasi ya tatu na Yanga Princess ya nne kutokana na tofauti ya mabao ya kufunga na kufugwa.

Mechi nyingine itakuwa ni Mkwawa Queens na The Tigers Queens katika Uwanja wa Chuo cha Mkwawa Iringa.



Wachezaji wa timu ya Wanawake ya Gofu ya Lugalo, wakipozi katika picha juzi baada ya mazoezi ya kujiandaa na mashindano ya Lugalo Ladies Open yatakayofanyika Mei 23, mwaka huu katika viwanja vya Gofu TPDF Lugalo, Dar es Salaam. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

# Yacouba mchezaji bora wa Februari Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Yanga, Yacouba Songne, raia wa Burkina Faso, amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwezi Februari wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa ni siku kadhaa tu baada ya kusajiliwa na Klabu ya Ihefu FC kwenye kipindi cha dirisha dogo, Januari.

Taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi, kupitia Idara ya Habari na Mawasiliano, imesema kuwa mchezaji huyo amechaguliwa baada ya kuwapiga kikumbo aliokuwa anagombea nao, mastraika wenzake Mnyarwanda Meddie Kagere wa Singida Big Stars na Mtanzania, Elius Maguri wa Geita Gold.

Imesema kuwa mchakato huo wa tuzo ya kila mwezi, umefanywa na Kamati ya Tuzo za Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF).

Kwa mwezi huo, mchezaji huyo alionyesha kiwango kizuri, ikiwa ni pamoja na kufunga mabao mawili, akihusika na upatikanaji wa bao moja kwenye michezo miwili aliyocheza.

Ihefu mwezi huo ilicheza mechi tatu, ikishinda miwili na kutoka sare moja, na Yacouba kwa kiasi kikubwa amehusika kuipandisha timu yake kutoka nafasi ya 11 hadi ya nane kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Takwimu zinaonesha kuwa amecheza mechi tatu na alitumia dakika 97 tu kupachika mabao mawili na 'assist' moja kwenye mechi za Ligi Kuu.

Mchezaji huyo alisajiliwa mwanzoni mwa Januari mwaka huu, akitokea Yanga ambako kwa muda mrefu alikuwa hachezi kutokana na kuwa majeruhi na hata alipopona hakuwa na namba kwenye kikosi cha kwanza cha timu hiyo, hivyo kutimkia Ihefu.

Kwa upande wa Maxime, aliwashinda Nasreddine Nabi wa Yanga na Fikirini Elias wa Coastal Union, ambapo kwa mwezi huo aliiongoza Kagera Sugar kucheza michezo matatu, ikishinda miwili dhidi ya Namungo bao 1-0, na ushindi kama huo dhidi ya Ruvu Shooting, ikitoka suluhu dhidi ya Polisi Tanzania, hivyo kujikusanyia pointi saba na kuipandisha timu yake kutoka nafasi ya saba hadi ya sita kwenye msimamo wa ligi hiyo yenye timu 16.

Kamati ya Tuzo pia imemchagua Meneja wa Uwanja wa Highland, Estates, uliopo Mbarali Mbeya, Omari Malile, kuwa meneja bora wa uwanja kwa mwezi huo.

## Onyango, Wawa wampa vitu Ame

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa zamani wa Simba, Ibrahim Ame, amesema anakoshwa sana na uchezaji wa mabeki wenzake, Joash Onyango wa Simba na Paschal Wawa wa Singida Big Stars kwani kila mmoja ana staili yake ambayo ilimfanya ajifunze vitu vingi kutoka kwao na kukomaa kiuchezaji.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ame, beki wa kati ambaye kwa sasa anaichezea KMC, amesema wakati akiwa Simba alikuwa na mabeki hao wote wawili, lakini kila mmoja alikuwa akimvutia kutokana na aina yake ya uchezaji.

Wakati Wawa anamvutia kutokana na upigaji wake wa mipira mirefu, anavutiwa na Onyango kutokana na aina yake ya upambanaji.

"Nikiwa pale Simba nilikuwa na mabeki wenzangu wa kigeni, Wawa na Onyango wakiwa wananivutia sana na ilibidi kuna vitu niinge kutoka kwao hadi hii leo.

"Kwa Wawa nimejifunza kupiga mipira mirefu, yule jamaa anapiga mipira mirefu tena kwa usahihi, na si kupiga tu, alijua wakati gani wa kuipiga kwa kina Maddie Kagere na Chris Mugalu, na pia anajua wakati gani wa kuanza mpira pembeni kwa kina Shomari Kapombe na Mohamed Hussein Tshabalala.

## Gofu wanawake kupigwa Mei Lugalo

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya wanawake ya mchezo wa gofu (Lugalo Ladies Open), yanatarajiwa kufanyika Mei 23-24, mwaka huu kwenye viwanja vya Gofu TPDF Lugalo, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, nahodha wa timu ya Gofu ya Wanawake ya Lugalo, Hawa Wanyeche, alisema mashindano hayo yanatajiwa kushirikisha nchi za Kenya, Uganda, Zambia pamoja na wenyeji, Tanzania.

"Baadhi ya nchi tayari tumezitumia mialiko ingawa mpaka sasa bado hawajatupa majibu, naamini mpaka mwishoni mwa mwezi huu tutakuwa tumepata majibu," alisema Wanyeche.

Alisema maandalizi kuelekea kwenye mashindano hayo yanaendelea vema kwani kila mchezaji anafanya mazoezi kwa lengo la kuuweka sawa mwili wake kabla ya kipute hicho kuanza na kwamba shughuli kubwa kwa sasa ni kutafuta wadhamini ambao watawasaidia ili mashindano hayo yaweze kufanyika kama yalivyopangwa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TIERNEY ATAKIWA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United inamtaka beki wa Arsenal kutoka Scotland, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 25, ambaye anaweza kugharimu zaidi ya pauni milioni 30. ***(Telegraph)***

### GVARDIOL ALENGWA LIVER
KLABU za Chelsea, Liverpool na Manchester City zinamlenga beki wa RB Leipzig na Croatia, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 21, msimu huu. ***(Fabrizio Romano)***

### NELSON MKATABA MPYA
ARSENAL ina imani winga wa England, Reiss Nelson, mwenye umri wa miaka 23, atakubali mkataba mpya katika klabu hiyo. ***(Mail)***

### OSIMHEN AWINDWA ARSENAL
ARSENAL pia inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 24, licha ya Manchester United kumtaka. ***(Rai, via Mirror)***

### BELLINGHAM NA UNITED
KIUNGO wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19, alikataa nafasi ya kukutana na wawakilishi wa Manchester United alipokuwa Birmingham City kwa vile hakutaka kukosa mazoezi. ***(Mail)***

### LAPORTE KUONDOKA CITY
MCHEZAJI Aymeric Laporte anataka kuondoka Manchester City msimu huu wa majira ya joto huku Barcelona wakiwa tayari kumnunua mlinzi huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 28. ***(Mundo Deportivo)***

### WARD-PROWSE AFIKIRIWA
KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Southampton, James Ward-Prowse, mwenye umri wa miaka 28. ***(Football Insider)***

### DE JONG BADO ATAKIWA
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag angependa kumsajili kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong, msimu huu, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, hataki kuondoka Barcelona. ***(Offside)***

### MAGUIRE KUUZWA
MLINZI wa England, Harry Maguire, mwenye umri wa miaka 30, ni miongoni mwa wachezaji kadhaa wa kikosi cha kwanza Manchester United ambao wako tayari kuuzwa msimu huu wa majira ya joto. ***(90min)***

### KENT ATAKIWA LEEDS
LEEDS United itachuana na Burnley kuwania saini ya Ryan Kent wakati mkataba wa winga huyo mwenye umri wa miaka 26 na Rangers utakapokamilika mwishoni mwa msimu. ***(Football Insider)***




## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR SASA KUMALIZIA MSIMU NJE YA UWANJA

Imependekezwa kufanyiwa operesheni ya kurekebisha mishipa ili kuepuka hatari kubwa kutokea...

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Neymar, atakosa kipindi kilichobaki cha msimu baada ya kutakiwa kufanyiwa upasuaji wa kurekebisha kifundo cha mguu na hiyo itamfanya kukaa nje ya uwanja kwa angalau miezi mitatu, klabu hiyo ya Ligue 1 imesema.

Neymar, ambaye ana mabao 13 na asisti 11 kwenye Ligue 1 msimu huu, hajacheza tangu alipotolewa nje kwa machela wakati timu yake iliposhinda 4-3 dhidi ya Lille mwezi uliopita, akikosa michezo miwili iliyopita ya PSG.

"Neymar Jr. amekuwa na vipindi kadhaa vya kuyumba katika kifundo cha mguu wa kulia katika miaka ya hivi karibuni," PSG ilisema katika taarifa.

"Kutokana na msukosuko wake wa mwisho Februari 20, imependekezwa operesheni ya kurekebisha mishipa ili kuepuka hatari kubwa kutokea tena. Wataalamu wote walioshauriwa wamethibitisha umuhimu huu.

"Kuchelewa kwa miezi mitatu hadi minne kunatarajiwa kabla ya kurejea mazoezini."

Kocha wa PSG, Christophe Galtier, alisema kukosekana kwa Neymar itakuwa pigo kubwa.

"Yeye ni mmoja wa wafungaji bora na mtoa usaidizi katika Ligue 1, kwa hivyo ni pigo kwetu," alisema Galtier akiwaambia waandishi wa habari.

"Bila Neymar, tunaweza kuwa na viungo wawili na washambuliaji watatu au viungo watatu na washambuliaji wawili. Kuna wachezaji ambao wanaweza kuingia nyuma kutoka kila aina ya nafasi."

PSG walisema atafanyiwa upasuaji huko Doha, Qatar.

Klabu hiyo iko kileleni mwa ligi ikiwa na tofauti ya pointi nane dhidi ya Marseille inayoshika nafasi ya pili.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,087,3
MECHI KALI
BAYERN MUNCHEN
VERSUS
PARIS ST GERMAIN
1 | 1.86
X | 3.94
2 | 3.36
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# FERNANDES HAFAI KUWA NAHODHA UNITED - SUTTON



**MANCHESTER, England**

BRUNO Fernandes hapaswi kuwa nahodha wa Manchester United tena baada ya kipigo cha aibu cha mabao 7-0 Jumapili kutoka kwa Liverpool, kwa mujibu nyota wa zamani wa England, Chris Sutton.

Mreno huyo, ambaye anaongoza timu hiyo kama kaimu wa nafasi ya nahodha wa klabu hiyo, Harry Maguire, alikosolewa kwa tabia na mtazamo wake katika mchezo huo.

"Kuna watu ambao wamehitimu zaidi kuwa nahodha," alisema Sutton.

"Fernandes si kiongozi wao bora. Kuna wengi wanaofaa zaidi yake, Casemiro akiwa mmoja."

Akizungumza kupitia BBC 5 Live ya Jumatatu usiku , mshambuliaji huyo wa zamani, alimpendekeza Raphael Varane kama chaguo linalofaa."

Kipigo hicho kilikuja siku saba baada ya Man United kushinda Kombe la Carabao - kombe lao la kwanza tangu kuwasili kwa Erik Ten Hag kama kocha Mei mwaka jana.

Wanashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu England na wametinga robo fainali ya Kombe la FA, pamoja na hatua ya 16-bora ya Ligi ya Europa.

Ten Hag, alielezea uchezaji wa timu yake dhidi ya wapinzani wao, Liverpool kama "usio wa kitaalamu."

# Felix na mustakabali wake Chelsea

**LONODN, England**

JOAO Felix amedokeza kwamba mustakabali wa kukaa muda mrefu na Chelsea unategemea na ushiriki wao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno, aliwasili hapo kwa mkopo akitokea Atletico Madrid katikati ya msimu.

Hata hivyo, ushindi wa Jumamosi dhidi ya Leeds United kwenye Ligi Kuu ulikuwa wa pili pekee kwa Chelsea katika mechi 12 kwa mwaka 2023 na wao wa kwanza tangu walipoifunga Crystal Palace Januari, na hivyo kuhitimisha msururu wa michezo sita bila kushinda.



Kikosi cha kocha Graham Potter kiko mbioni kuwinda mchujo wa kumaliza katika nafasi nne za juu za kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, wakiwa wamejikusanyia pointi 11 nyuma ya Tottenham walio nafasi ya nne.

Wakati Joao Felix alionesha furaha yake pale Stamford Bridge, alipendekeza kukubali kwa mkataba wa kudumu kunategemea ikiwa wanaweza kubadilisha msimu wao.

"Kuhusiana na kama ninataka kubaki au la, nadhani siku zijazo, hakuna anayejua. Sasa ninaangazia tu michezo ya mbele," alisema katika mkutano na waandishi.

"Baada ya hapo, hatujui nini kitatokea. Lakini nina furaha hapa. Klabu ni kubwa sana, inashangaza, kila mtu nyuma ya klabu ni mzuri hivyo ndiyo nina furaha kuwa hapa.

"Kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya siku zote ni tofauti. Ni mashindano ambayo kila mtu anataka kucheza.

"Kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya ni uamuzi muhimu. Lakini siku zijazo, hakuna anayejua kwa hiyo tusubiri kitakachotokea."

## HABARI MICHEZO

# 305,640/-




Mshindi wa Jackpot Bonus ya SportPesa, Kenedy Kellya, kutoka Mlandizi mkoani Pwani akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 10 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 15 kati ya 17 kwenye Supa Jackpot wiki iliyopita. **MPIGAPICHA WETU**

# FUNDI UJENZI ALAMBA MILIONI 10/- JACKPOT BONUS YA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

FUNDI ujenzi wa kuezeka nyumba kutoka Mlandizi Stendi mkoani Pwani, Kenedy Kellya, ameibuka na kitita cha Sh. 10,124,322 katika Supa Jackpot Bonus ya SportPesa ya mwishoni mwa juma baada ya kupatia kwa usahihi mechi 15 kati ya 17 za Supa Jackpot.

Akizungumza katika ofisi za SportPesa Oysterbay, Dar es Salaam, Kellya alisema alianza kucheza na SportPesa Septemba mwaka jana baada ya kushawishika na washindi wa SportPesa waliokuwa wakitangazwa.

"Nilianza kucheza na SportPesa mwaka jana mwezi kama wa tisa, baada ya kushawishika na namna nilikuwa naona washindi wa SportPesa wakiwa wanatangazwa kupitia mitandao ya kijamii, taarifa za habari na kwenye magazeti," alisema.

Kellya alisema baada ya kushawishika alimuomba rafiki yake (ambaye hakutaka kumtaja jina), amsaidie kupakua App ya SportPesa na kisha alianza kucheza bila kukata tamaa.

"Mimi wakati naanza kucheza kwa mara ya kwanza nilikuwa nacheza michezo ya Casino. Katika kucheza michezo hiyo ya Casino nimewahi kushinda laki tatu ambazo zilinitia moyo wa kuwa naweza kupata zaidi," alisema Kellya.

Akizungumzia mkeka wake wa Supa Jackpot ulioshinda Kellya alisema kwanza yeye si mchezaji wa mara kwa mara wa ubashiri wa mpira. Lakini anajitahidi mara kwa mara kucheza Jackpot za SportPesa kila anapopata nafasi.

"Nikikusimulia kuhusu huu mkeka unaweza kushangaa. Siku niliyoweka huu mkeka uliyoshinda ilikuwa Jumatano iliyopita. Nilikuwa kijiweni pale Mlandizi Stendi nikamwomba rafiki yangu mmoja anipe hela niweke mkeka wa Supa Jackpot".

"Mshikaji alinipa Sh. 5,000 mara baada ya kuuweka huu mkeka ukatokea ubishani mkubwa sana. Niliwaambia washikaji zangu waweke mkeka kwa kuufuatisha na walikataa na kuniambia haya mambo ya ubashiri ni uongo, watu wanapangwa na hata nikishinda sitalipwa."

Anaendelea kusema siku ya Jumamosi alifuatilia matokeo na kukuta amepatia kwa usahihi mechi 10 za Supa Jackpot kati ya 17. Baada ya hapo hakufuatilia tena mpaka ilipofika Jumatatu asubuhi, akiwa yeye na mkewe alichukua simu kutoka kwenye chaja na kukuta sms ya hongera.

"Nafikiri asubuhi ya Jumatatu itabaki kwenye kumbukumbu zangu kwa muda mrefu. Cha kwanza sikutarajia kushinda kiwango hiki cha fedha. Cha pili baada ya kuona sms nilimwonyesa mke wangu nikamwambia nimeshinda, lakini kwa muda ule 'wenge' lilishaaanza kuniingia mpaka kiwango nilichoshinda nikawa sikiamini.

"Mke wangu alinithibitishia mara mbili mbili kwamba nimeshinda milioni 10 ila baada ya makato ni milioni tisa. Bado sikuamini hivyo nilitoka na kwenda moja kwa moja 'maskani' pale stendi na kumuonyesha jamaa yangu mmoja (jina kapuni), ambaye yeye ana kibanda cha kuonyesha mpira.

"Wakati nafika nikapokea simu kutoka SportPesa Kitengo cha Huduma kwa wateja wakinitaarifu kwamba natakiwa nifike ofisi kwao ili suala langu lishughulkiwe."

Kellya anamalizia kwa kusema baada ya kupitia hatua zote na kujiridhisha, anawaasa Watanzania kuiamini SportPesa kwani malipo ni papo hapo na pia wasikate tamaa waendelee kucheza kwani hakuna aijuaye siku yake.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano SportPesa, Sabrina Msuya, alimpongeza Kellya na kumtaka akawe balozi mzuri wa SportPesa na pia aendelee na moyo huo huo alionao wa kuwafundisha Watanzania wenzake, ili na waweze kushinda.

"Nikupe hongera kwa kushinda Supa Jackpot Bonus ya milioni 10. Wewe ni mmoja kati ya washindi wengi ambao wanashinda kila wiki na kila siku. Supa Jackpot yetu wiki hii imesimamia Sh. 1,087,305,640," alisema.

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/03/23 | 18:00 | Everton FC vs Brentford FC | 2.55 | 3.05 | 2.70 |
| 02. 11/03/23 | 18:00 | Preston North End vs Cardiff City | 2.55 | 3.10 | 2.70 |
| 03. 11/03/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Watford FC | 2.65 | 3.15 | 2.50 |
| 04. 11/03/23 | 18:15 | Elche CF vs Real Valladolid | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 05. 11/03/23 | 18:30 | FC Pacos Ferreira vs Santa Clara Azores | 2.31 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 11/03/23 | 20:15 | KAS Eupen vs KV Oostende | 2.46 | 3.30 | 2.60 |
| 07. 11/03/23 | 22:45 | Bologna FC vs Lazio Rome | 2.95 | 3.15 | 2.29 |
| 08. 11/03/23 | 23:00 | Sparta Rotterdam vs Vitesse Arnhem | 2.35 | 3.25 | 2.80 |
| 09. 12/03/23 | 14:15 | NEC Nijmegen vs FC Utrecht | 2.45 | 3.20 | 2.70 |
| 10 12/03/23 | 14:30 | US Lecce vs Torino FC | 2.85 | 2.90 | 2.55 |
| 11. 12/03/23 | 16:00 | RCD Mallorca vs Real Sociedad San Sebastian | 3.20 | 2.85 | 2.36 |
| 12. 12/03/23 | 17:00 | AC Ajaccio vs Montpellier HSC | 2.75 | 3.10 | 2.50 |
| 13. 12/03/23 | 17:00 | FC Nantes vs OGC Nice | 3.05 | 3.10 | 2.28 |
| 14. 12/03/23 | 17:00 | Hellas Verona vs AC Monza | 2.36 | 3.05 | 2.95 |
| 15. 12/03/23 | 18:30 | Rio Ave FC vs Gil Vicente Barcelos | 2.28 | 3.10 | 3.05 |
| 16. 12/03/23 | 20:30 | KRC Genk vs Union Saint-Gilloise | 2.29 | 3.40 | 3.05 |
| 17. 12/03/23 | 21:30 | VfL Wolfsburg vs Union Berlin | 2.26 | 3.20 | 3.30 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 08/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1636 | Sagan Tosu vs Consadole Sapporo | 2.51 | 3.27 | 2.53 |
| 13:00 | 1653 | Vissel Kobe vs Nagoya Grampus | 2.21 | 3.11 | 3.06 |
| 13:00 | 1952 | Shonan Bellmare vs Urawa Red Diamonds | 2.53 | 3.16 | 2.58 |
| 13:00 | 2269 | Cerezo Osaka vs FC Tokyo | 2.17 | 3.16 | 3.11 |
| 13:00 | 3849 | Avispa Fukuoka vs Niigata Albirex | 2.13 | 3.07 | 3.28 |
| 13:00 | 3852 | Kashiwa Reysol vs Kashima Antlers | 2.75 | 3.32 | 2.30 |
| 13:00 | 4680 | Kyoto Sanga vs Gamba Osaka | 2.34 | 3.16 | 2.80 |
| 13:00 | 4728 | Yokohama F Marinos vs Jubilo Iwata | 1.28 | 5.17 | 7.86 |
| 13:00 | 5741 | Shimizu S Pulse vs Kawasaki Frontale | 3.73 | 3.57 | 1.81 |
| 13:00 | 5812 | Sanfrecce Hiroshima vs Yokohama | 1.32 | 4.66 | 7.66 |
| 14:30 | 2270 | Erzurum BB vs Keciorengucu | 2.67 | 3.14 | 2.40 |
| 14:30 | 4027 | Manisa BBSK vs Bodrumspor | 2.52 | 3.14 | 2.53 |
| 16:00 | 1686 | Ethiopia Electricity vs Bahir Dar Kenema FC | 4.36 | 3.06 | 1.84 |
| 16:00 | 1698 | Croatia Zmijavci vs NK Dubrava | 2.62 | 3.03 | 2.51 |
| 16:00 | 2309 | FC Struga Trim Lum vs Shkupi Skopje | 3.38 | 2.81 | 2.23 |
| 16:00 | 3006 | FK Loznica vs Metalac | 2.67 | 3.08 | 2.43 |
| 16:00 | 3206 | Tabor Sezana vs NK Rogaska | 1.79 | 3.52 | 3.88 |
| 16:00 | 4515 | FK Skopje vs Makedonija GjP | 3.84 | 2.85 | 2.04 |
| 16:00 | 5308 | Shkendija vs Rabotnicki Sk | 1.37 | 4.23 | 7.43 |
| 16:00 | 5551 | Akademija Pandev vs Pobeda Junior | 1.31 | 4.65 | 8.07 |
| 16:15 | 1655 | Al Orubah vs Al Jabalain | 2.49 | 2.83 | 2.83 |
| 16:30 | 2038 | Liptovsky Mikulas vs MFK Skalica | 2.55 | 3.15 | 2.55 |
| 17:00 | 5022 | Jezero vs Mornar Bar | 1.74 | 3.26 | 4.56 |
| 17:00 | 5834 | FK Arsenal Tivat vs Buducnost | 5.61 | 3.69 | 1.54 |
| 17:30 | 1768 | Kustosija vs Orijent Rijeka | 2.32 | 3.20 | 2.73 |
| 18:00 | 5813 | NK Aluminij vs NK Fuzinar Ravne | 1.38 | 4.34 | 6.82 |
| 18:30 | 1960 | Bahrain Club vs Al Shabbab | 3.01 | 2.95 | 2.33 |
| 18:30 | 2306 | Al Hala Muharraq vs Manama Club | 5.58 | 3.51 | 1.57 |
| 18:30 | 5400 | Atromitos vs AEK Athens | 7.45 | 4.26 | 1.42 |
| 19:00 | 2198 | Adama City FC vs Fasil Kenema | 4.46 | 3.32 | 1.74 |
| 19:00 | 3687 | Parnu JK Vaprus vs Trans Narva | 3.21 | 3.47 | 2.00 |
| 19:00 | 3741 | Ismaily SC vs Farco FC | 2.56 | 2.71 | 3.07 |
| 19:00 | 4211 | Paide Linnameeskond vs Levadia Tallinn | 2.34 | 3.25 | 2.74 |
| 20:00 | 1410 | Nomme Kalju vs Flora Tallinn | 4.55 | 3.83 | 1.61 |
| 20:00 | 1486 | Lamia vs PAOK | 8.28 | 4.14 | 1.36 |
| 20:00 | 2140 | Sutjeska vs Decic Tuzi | 1.66 | 3.58 | 4.57 |
| 20:00 | 3638 | Genclerbirligi vs Denizlispor | 1.71 | 3.54 | 4.10 |
| 20:00 | 4946 | Petrovac vs Rudar Pljevlja | 1.84 | 3.16 | 4.14 |
| 20:30 | 1628 | Partizan vs Kolubara | 1.18 | 5.75 | 11.29 |
| 20:30 | 4820 | Dondol Stars vs Amazulu | 6.43 | 4.25 | 1.41 |
| 20:45 | 3566 | Sonderjyske vs Silkeborg | 3.21 | 3.47 | 2.00 |
| 20:45 | 5155 | Wisla Plock vs Warta Poznan | 2.62 | 2.98 | 2.54 |
| 21:30 | 1894 | Guarany CE vs Crato EC CE | 1.83 | 3.21 | 4.14 |
| 21:30 | 2180 | Itapipoca EC CE vs Pacatuba EC CE | 2.34 | 2.70 | 2.90 |
| 21:30 | 2282 | Pague Menos CE vs Icasa CE | 3.16 | 2.90 | 2.28 |
| 22:45 | 3143 | Livingston vs Dundee Utd | 2.16 | 3.22 | 3.22 |
| 22:45 | 3220 | Hibernian vs Rangers | 5.20 | 4.10 | 1.54 |
| 22:45 | 3475 | Celtic vs Hearts | 1.17 | 6.80 | 12.00 |
| 23:00 | 2684 | Bayern Munchen vs Paris St Germain | 1.86 | 3.94 | 3.36 |
| 23:00 | 2971 | Tottenham vs AC Milan | 1.90 | 3.40 | 3.70 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Machi 8, 2023

Nipashe



UKURASA 21

**Neymar sasa kumalizia msimu nje ya uwanja**

# YANGA SC: BAMAKO HAWATOKI LUPASO LEO

## ●●●Nabi ataja pakuishika, wenyewe waonya wasema wamefuata pointi tatu, lakini...

**Na Saada Akida**

WAKATI wawakilishi wa nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, Yanga, wakiikaribisha Real Bamako ya Mali katika Uwanja wa Benjamin Mkapa leo, Kocha Mkuu wa vinara hao wa Ligi Kuu Bara, Nasreddine Nabi, amesema tayari amekiandaa vema kikosi chake kwa ajili ya kupata matokeo katika mchezo huo wa marudiano utakaopigwa majira saa 1:00 usiku.

Timu hizo zinakutana leo uwanjani hapo baada ya Jumapili ya Februari 26, kutoka sare ya bao 1-1 nchini Mali, matokeo ambayo yameiweka Yanga katika nafasi ya pili kwenye Kundi D, ikiwa na pointi nne nyuma ya vinara US Monastir ya Tunisia yenye alama saba, huku TP Mazembe ya DR Congo ikishika nafasi ya tatu kwa pointi zake tatu na Real Bamako ikiburuza mkia kwa pointi mbili ilizojikusanyia hadi sasa.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nabi akizungumza na Nipashe jana, alisema watakosa huduma ya wachezaji wao wawili, Jesus Moloko ambaye ni majeruhi na Salum Abubakari 'Sure Boy', aliyepata msiba wa mtoto wake.

Alisema mbali na wawili hao, wachezaji wote wako vizuri na tayari kupambana kwa ajili ya mchezo wa leo ili kupata matokeo mazuri na kuvuna pointi tatu zitakazowaweka katika nafasi nzuri ya kufuzu robo fainali.

"Real Bamako tulicheza nao hivi karibuni na tunarudiana nao kesho (leo), baada ya mchezo huo pia tunacheza na US Monastir katika uwanja wetu wa nyumbani.

"Tunahitaji kushinda mechi zote mbili na zote ni ngumu, ili tufuzu tushinde mechi ya leo halafu dhidi ya US Monastir kwa sababu ya kutafuta pointi zote sita katika uwanja wa nyumbani," alisema Nabi.

Alisema wachezaji hawakufurahia matokeo waliyoyapata Mali kwa wapinzani wao kusawazisha dakika za mwisho, hali ambayo iliwaumiza hivyo kuelekea mchezo wa leo morali ya kupata matokeo mazuri ipo juu.

"Real Bamako hawakuja kutalii, wako nchini kwa lengo la kutafuta matokeo mazuri kwa hali hiyo, tumejiandaa vizuri kuhakikisha tunapata matokeo mazuri katika uwanja wa nyumbani.

"Tumefungwa jumla ya mabao nne katika mechi tatu kwa staili moja ya kona, hii yote ni kutokana na wachezaji wangu kutokuwa makini na mawasiliano kuwa madogo uwanjani," alisema na aliongeza:

"Hii nimelifanyia kazi mazoezini kuhakikisha tatizo hilo linaondoka na kuwataka wachezaji kuwa makini uwanjani," alisema Nabi.

Mwakilishi wa Wachezaji wa Yanga, Ibrahim Abdallah 'Bacca', alisema wako vizuri na wamejiandaa kwa ajili ya kutafuta ushindi katika mchezo wao huo.

Alisema licha ya kutafuta ushindi katika mchezo huo, lakini wanahitaji ushindi kwa ajili ya kumfariji mchezaji mwenzao Sure Boy aliyempoteza mtoto wake.



Mayele

"Benchi la ufundi limefanya kazi yake, jukumu kubwa limebaki kwetu kutimiza kile tulichopewa katika mazoezi ikiwamo umakini katika makosa ya mipira ya kona ambayo tulifungwa kwenye michezo mitatu iliyopita," alisema Bacca.

Kocha Mkuu wa Real Bamako, Nouhoum Diane, alisema wanajua ugumu wa mchezo wa leo dhidi Yanga, lakini kitu kizuri kwao wanakwenda kukutana na timu ambayo wanaijua vizuri.

"Nimchezo mgumu kwa sababu Yanga wapo nyumbani, lakini faida kubwa tuliyonayo nikujua mbinu zao na mapungufu waliyokuwa nayo kwa hiyo tutapambana kuhakikisha tunapata ushindi," alisema Diane.

Kocha huyo alikiri kwamba pamoja na kikosi chake kutokuwa na uzoefu mkubwa katika mashindano hayo, lakini watajitahidi kucheza kwa mipango ili kumaliza mechi za makundi katika nafasi nzuri.

Alisema katika Kundi D hakuna timu dhaifu, hivyo licha ya kushindwa kupata ushindi katika mechi tatu za mzunguko wa kwanza, bado anayo matumaini ya kufanya vizuri kwa sababu idadi ya pointi walizopishana ni ndogo.

## Opa wa Simba Queens atua Besiktas ya Uturuki

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA hatari wa timu ya wanawake ya Simba Queens na Timu ya Taifa ya Tanzania, Twiga Queens, Opa Clement, amejiunga na Klabu Besiktas ya Uturuki.

Taarifa iliyotolewa jana na Klabu ya Simba, imesema uongozi wa klabu hiyo umefikia makubaliano na klabu hiyo ya Uturuki, kumuuza nahodha wao na kinara wa mabao wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, huku akiwa ndiyo mfungaji bora wa msimu uliopita.

"Uongozi wa klabu ya Simba umefikia makubaliano ya kumuuza nahodha wa timu yetu ya Simba Queens, Opa Clement kwenda Besiktas ya Uturuki.

"Tayari mshambuliaji huyo kinara ameshaondoka nchini kuelekea Uturuki kwenda kuanza maisha mapya ya soka katika timu yake ya Besiktas.

"Mpaka Opa anaondoka Ligi ya Wanawake mzunguko wa kwanza ukiwa umemalizika, yeye ndiye kinara wa ufungaji akiwa amepachika wavuni mabao tisa.

"Uongozi wa Klabu ya Simba unamtakia kheri Opa katika majukumu yake mapya na pia unamkaribisha muda wowote atakapoamua kurejea tena nyumbani," ilieleza taarifa hiyo.

Hii si mara ya kwanza kwa mchezaji huyo kuondoka, kwani Machi mwaka jana, alikwenda Klabu ya Kayserispor Girl kwa kile kilichoelezwa kufanya majaribio na kama angefanikiwa klabu hiyo ingekaa mezani na Simba kumalizana, lakini alirejea nchini baadaye na haikufahamika kama alifuzu au la.

Lakini pia hii si mara ya kwanza kwa Simba Queens kufanya hivyo kwani Machi 2021, ilimuuza aliyekuwa nahodha wake wakati huo, Mwanahamisi Omari kwenda Klabu ya Shabab Atlas ya Morocco, lakini kwa sasa amerejea tena klabuni hapo katika kipindi cha dirisha dogo la usajili.

Mchezaji mwingine ni kiungo, Flavian Mawete Musolo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo aliyeichezea mwaka 2020 hadi 2021 akauzwa kwenda Klabu ya Adana Idmanyurduspor ya Uturuki anayoichezea hadi leo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >